**CAG** Zanzibar akubali yaishe, aomba radhi

UKURASA 18



**Mtetezi** wa haki, mwasisi TAMWA afariki dunia

UKURASA 18




UKURASA 11

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumanne Juni 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581340
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Viongozi wa dini wajitosa Bandari

**• Wateta** kwa saa saba na waziri, TPA; waweka msimamo... *Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wabunge kutaka kuunga mkono kila kitu bila kuhoji ni kuwanyima wananchi haki yao ya kulinda rasilimali za Taifa.

**Padri Charles Kitima**

Serikali imeichukua DP World kutokana na uzoefu wake katika masuala ya bandari barani Afrika.

**Mbarawa**

Umma uelimishwe kuhusu mkataba huo na namna maslahi ya nchi yatakavyolindwa.

**Sheikh Nuhu Mruma**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**DC AAGIZA KUFICHULIWA WANAOJIHUSISHA NA MAPENZI YA JINSIA MOJA**
MKUU wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni, amewataka viongozi wa dini, kimila na...

UKURASA WA 4
RIPOTI YA UCHUNGUZI-2
**APOKWA NG'OMBE 170, MILIONI 17/- KINYAMA**
SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilianika simulizi ya ukatili dhidi ya wanakijiji...

UKURASA WA 5
**KUNDI LA WANAUME KUFIKIRIWA MIKOPO YA MAKUNDI MAALUM**
BUNGE limeelezwa kuwa serikali inaangalia uwezekano wa kuweka kundi la wanaume...

## Mahakama yaelezwa mwanafunzi wa UDOM alivyouawa

UKURASA 3

## Vigogo wa zamani CWT wafichua kiini migogoro

UKURASA 2

**MICHEZO** **AZAM FC SI KWA YANGA** UK.24 **KABWELA** UK.7



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mratibu wa Kimataifa wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani katika mwitikio wa kupambana na Ukimwi (PEPFAR) na Mwakilishi Maalum wa Serikali ya Marekani katika masuala ya Diplomasia ya Afya, Balozi Dk. John Nkengasong, pamoja Mtendaji Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria, Peter Sands, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Viongozi wa dini wajitosa Bandari

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini mbalimbali jana walijifungia kwa takribani saa saba, wakijadiliana na serikali kuhusu maslahi ya nchi katika mikataba ya kuziendesha bandari.

Kikao hicho kilifanyika jana jijini Dar es Salaam kwa kuzingatia ibara saba za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Baada ya kikao hicho ambacho kilihudhuriwa na viongozi waandamizi wa dini za Kikristo na Kiislamu pamoja na timu ya serikali iliyoongozwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, viongozi hao waliishauri serikali kurekebisha baadhi ya vifungu vya mkataba wa ushirikiano kati yake na Dubai (IGA).

Lengo ni kulinda maslahi ya umma katika mikataba itakayoingiwa kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na kampuni ya DP World ya Dubai.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa majadiliano hayo, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Charles Kitima, alisema wameishauri serikali kuwa makini katika mikataba hiyo ili isihatarishe rasilimali nyingine za nchi, pale itakapotokea mgogoro baina ya TPA na DP World.

Alisema wameomba kuona mikataba itakayosainiwa kati ya TPA na mwekezaji huyo, kwa kuwa mjadala wa IGA na azimio la Bunge, uliibua maswali na wasiwasi kutoka kwa wananchi.

"Kwa mfano hii ni kampuni mfanyabiashara (DP World). Kumbukeni Tanzania imeingia kwenye migogoro ya ndege zetu kukamatwa kwa sababu kampuni fulani tuliikosea kama nchi, lakini wenzetu walichofanya wanaunda kampuni badala ya serikali moja kwa moja... kwa hiyo tatizo likitokea shida inakuwa ya kampuni siyo ya nchi," alisema Padri Kitima.

Aliongeza: "TPA ni serikali siyo kampuni ya biashara. Kwa hiyo, unapoishtaki bado serikali inashtakiwa kama nchi... hivi ndio tukasema wafikirie namna ya kuangalia nchi tunaiwekaje salama."

Alisema kipengele kingine walichoshauri kirekebishwe kabla ya kuingia kwenye mikataba ni kinachoinyima serikali uhuru wa kuboresha bandari zingine bila ruhusa ya mwekezaji huyo.

"Hii nchi ni yetu, wewe (DP World), umechukua gati mbili, tatu bandari ya Dar es Salaam usiniambie ninapotaka kuendeleza bandari ya Kilwa lazima nikutaarifu, wewe nani?" Alihoji.

Alisema kipengele hicho kinapaswa kurekebishwa, ili serikali isijifunge mikono katika kutafuta mwekezaji mwenye uwezo katika masuala mahsusi kwa maslahi ya nchi.

"Vifungu vilikuwa vingi, vingine vina makosa madogo madogo ambayo yalikuwa na lugha ya kitaalamu inayoibana nchi na hivyo wameviona watavishughulikia," alisema.

Padri Kitima alisema baada ya uchambuzi wa kina, viongozi hao wameunda kamati ndogo itakayowasilisha maoni yake serikalini, ili kuweka marekebisho yanayohitajika.

"Katika hiyo mikataba ya kikazi tumewaomba rasmi, tunaomba na hiyo tuione kwa sababu kama wananchi walikuwa na shaka... sio kusema kutakuwa na 'local content' sijui na nini na nini hapana, tunataka tuone ajira na maslahi ya nchi yanalindwa," alisema.

Awali, Padri Kitima alisema kikao hicho kimeitishwa kwa kuzingatia ibara saba za Katiba ambazo ni za 8, 9, 18, 19, 20, 27 na 28; ambazo pamoja na mambo mengine zinawataka wananchi kutunza na kulinda rasilimali za nchi na pia kuisimamia serikali.

Akifungua kikao hicho, Waziri Mbarawa alisema serikali imeichukua kampuni ya DP World kutokana na uzoefu wake katika masuala ya bandari barani Afrika na uwezo wa kitaalamu iliyonao.

**BUNGE**

Kuhusu Bunge, Padri Kitima alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza umuhimu wa mikataba kuzingatia maslahi ya nchi, hivyo baadhi ya wabunge kutaka kuunga mkono kila kitu bila kuhoji ni kuwanyima wananchi haki yao ya kulinda rasilimali za Taifa.

"Mkataba kama haulindi maslahi ya nchi halafu wewe unasema lazima uungwe mkono una maana gani?" alihoji.

Alisema kama wabunge wangekuwa wanathamini wananchi, wasingetoa siku moja ya kwenda Dodoma kutoa maoni kuhusu IGA. "Nadhani Bunge lijitafakari."

Alisema kumekuwa na maswali kuhusu baadhi ya wabunge kuingia bungeni kwa tiketi yenye maswali, hivyo katika uchaguzi ujao serikali ihakikishe wananchi wanapata wawakilishi wenye sifa stahiki.

Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Nuhu Mruma, aliishauri serikali kuendelea kuelimisha umma kuhusu mkataba huo na namna maslahi ya nchi yatakavyolindwa.

Viongozi wa dini waliohudhuria kikao hicho ni Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuber, Rais wa TEC, Askofu Gervas Nyaisonga, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Stanley Hotay, Askofu Mkuu wa KKKT, Dk. Alex Malasusa, masheikh, maaskofu, wachungaji na mapadri.

**SAMIA: NCHI HAIUZWI**

Akiwahutubia wananchi baada ya kuwasili jijini Mwanza jana, Rais Samia Suluhu Hassan alisema hakuna mpango wowote wa kuigawa nchi na kuwataka Watanzania kuwa watulivu kwa kuwa maslahi ya nchi yanazingatiwa.

"Tanzania ni moja, haiuziki wala haigawanyiki. Kwa hiyo, ndugu zangu Mama ni Mtanzania, maendeleo yetu ni muhimu na kila kinachofanyika ni kwa maendeleo ya Taifa na Watanzania kwa ujumla," alisema.

***Imeandikwa na Restuta James (DAR) na Vitus Audax (MWANZA)**

## Rais mstaafu aeleza kiini sarakasi CWT

**Na Waandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Gratian Mukoba, amesema kuyumba kwa chama hicho kwa miaka ya hivi karibuni, kunatokana na mambo kadhaa, ikiwamo wanaopewa dhamana kukisimamia chama kutoonyesha dhamira ya uongozi na nia thabiti kutetea maslahi ya waajiriwa.

Wakati Mukoba akitoa kauli hiyo, Mjumbe wa Kamati Tendaji Taifa, Thobias Sanga, amesema kiini cha migogoro ni viongozi kutotimiza wajibu, kusigina Katiba, miongozo na maslahi binafsi

Mukoba aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe iliyotaka kufahamu mbinu alizozitumia akiwa kiongozi wa chama hicho kuimarisha umoja huo na kutetea maslahi ya waajiriwa.

"Chama cha wafanyakazi hakiongozwi kama kampuni binafsi. Kina misingi, katiba, kanuni, sheria. Sasa hawa watu wanataka kukiendesha chama kama kampuni, ndiyo maana wanakwama kila siku.

Mukoba ambaye aliwahi Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), alisema malalamiko kutoka kwa wanachama kwenda kwa uongozi wa chama, hutokana na uongozi kutokuwa upande wa mwanachama.

Alisema kiongozi yeyote anayelenga kuwakomboa na kutetea anaowaongoza, husimamia misingi na si maslahi binafsi na kuegemea upande wa mwajiri na kuunda mazingira ya urafiki, yanayojenga vikwazo vya utetezi wanachama.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za CWT Mkoa wa Njombe jana, Sanga alisema miongozo ingefuatwa kusingefikia hatua hiyo mbaya.

"Naona kama watu wametanguliza maslahi binafsi, kama watu wanafika wanakataa kutumwa kazi na mwajiri mkuu wa nchi, basi kuna maslahi binafsi, lakini ni uhuru wao, ninadhani tungefuata miongozo yetu tusingefikia hatua hii mbaya ambayo tumefikia," alisema.

Aliwasihi viongozi wa chama hicho nchini kutotumia mitandao ya kijamii kushawishi watu, kurubuni, kusema uongo na kuchafuana, akiitaja sio njia nzuri ya kutatua mgogoro.

"Kwa mfano kamati ya utendaji tuna wajumbe 32, juzi wajumbe 18 tulifanya kikao na wawili ambao hawakuwapo tupo kundi moja, wale wengine hawakuungana na sisi, lakini juzi kwenye mkutano na waandishi baadhi waliungana na viongozi wa sasa ambao wanafanya ubadhirifu," alidai Sanga.

Mwenyekiti wa CWT Njombe, Valian Ngalioma, alishauri kamati tendaji mikoa yote kuungana kuwasimamia viongozi kufanya kazi waliyotumwa na sio vinginevyo.

Chama hicho kina wanachama 247,860. Kati yao, wanawake ni 113,645 kwa mujibu wa tovuti ya CWT, kikiongozwa na Rais Leah Ulaya.

Chama hicho kiliundwa mwaka 1993 kwa lengo la kutetea na kukuza haki za wanataaluma hiyo nchini.

***Imeandikwa na Christina Mwakangale (DAR) na Elizabeth John, NJOMBE**

# Mahakama yaelezwa mwanafunzi UDOM alivyouawa kwa kunyongwa

Na Grace Gurisha

SAJENTI Emmanuel Francis ameieleza mahakama jinsi fundi wa A/C za magari, Idrisa Mwakabola (22), alivyomuua mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Happiness Fredrick (22) kwa kumnyonga, baada ya kumuhisi kuwa ana mahusiano ya kimapenzi na mtu mwingine.

Aidha, alidai kuwa kabla ya kufanya mauaji hayo alimpeleka Happiness, Kariakoo kwa ajili ya kununua nguo (suruali za kike za kubana yaani taiti) kwa ajili ya maandalizi ya safari ya kurudi chuoni Dodoma.

Sajenti Francis alidai hayo jana mbele ya Jaji Ephery Kisanya katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Kivukoni Dar es Salaam, wakati akitoa ushahidi dhidi ya Mwakabola, anayetuhumiwa kumuua kwa makusudi Happiness, Machi 18, 2019.

Alidai kuwa alipata taarifa kutoka kwa msiri kwamba kuna mtu ambaye ni rafiki wa karibu na marehemu, aliyewahi kufika msibani akiwa wa kwanza hali iliyoshangaza alipata wapi taarifa za msiba wa Happiness hadi kuwa wa kwanza.

Sajenti Francis alidai taarifa hizo alizipata akiwa msibani, kwa hiyo alimfuata baba wa marehemu, Fredrick Francis na kumweleza alichokifuata hapo msibani na kudai kuwa mtu huyo alipigiwa simu na alitaka kujua ni nani.

Shahidi huyo alidai kuwa alimpata mtu huyo aliyepigiwa simu aliyemtaja kwa jina moja la Dorice na alimchukua na kwenda naye hadi Kituo cha Polisi Chang'ombe kwa ajili ya mahojiano, kujua aliyempigia simu.

"Dorice katika mahojiano alieleza kwamba aliyempigia simu kumpa taarifa za msiba wa Happiness ni Idrisa, nilimwomba Dorice afanye mawasiliano ambapo alimwahidi kwamba atakuja kuaga mwili nyumbani," alidai.

Alidai kuwa Machi 21, 2019 mwili wa marehemu ulichukuliwa kutoka nyumbani hadi Kanisa la Roma Buza kwa ajili ya kuaga, wakati shughuli hiyo inaendelea, Dorice aliendelea kuwasiliana na Idrisa na alipofika alimweleza kwamba hawezi kuingia kanisani kwa sababu yeye ni Muislamu.

"Nilimwelekeza Dorice kuwa atoke nje wakati anaelekea kwenye geti la kanisa, Idrisa aliingia ndani na alipofika ndani ya kanisa alikumbatiana na mama mmoja na kisha kupanga foleni ya kuaga ndipo nilipokaa nyuma yake na alipofika mlangoni ili atoke nje nilimshika bega."

"Nikumweleza kwamba dogo nina shida na wewe naomba tuongee, alishtuka sana akataka kukimbia kwa sababu tayari tulikuwa tumeshajipanga, tukamkamata na kumwingiza ndani ya gari na kumpeleka Kituo cha Polisi Chang'ombe," alidai.

Sajenti Francis aliendelea kudai kuwa walipofika kituoni alimuhoji Idrisa na alikiri kufanya tukio hilo la mauaji na kumweleza sababu ya kufanya hivyo ni wivu wa mapenzi.

Alidai kuwa Idrisa alimweleza kwamba Machi 18, 2019 aliwasiliana na marehemu kuwa anataka kurudi chuoni masomoni, walikubaliana wakutane eneo la Shaurimoyo ambalo mshtakiwa anafanyia shughuli zake za ufundi wa A/C za magari.

"Baada ya hapo waliingia Kariakoo kufanya manunuzi ya nguo yaani suruali za kike za kubana, walipotoka hapo walikwenda stendi ya Ubungo kukata tiketi, walikata tiketi ya basi Kimbinyiko, baada ya kukata tu, marehemu alipokea simu kutoka kwa mtu aliyehisi kwamba ana mahusiano naye ya kimapenzi," alidai.

Alidai kuwa hapo ndipo nia ovu ikaanza kutendeka, alienda naye hadi nyumbani kwao Kigamboni Mji Mwema, walipofika waliingia chumbani na yeye alienda kumnunulia juice, akamwekea kidonge cha usingizi, Happiness akalala ndipo alipotimiza haja yake kwa kumnyonga hadi kufa.

"Alimbeba marehemu kwa kushirikiana na mama yake mzazi na kumwingiza ndani ya gari kwa madai kwamba anampeleke hospitali, lakini alikwenda kumtupa, basi hapo ndipo nilipoishia, taratibu zingine za kuandaa jalada zikaendelea," alidai.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**Tarehe 13/06/2023**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumanne** tarehe **13/06/2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

Gari hizo zenye namba za usajili:
**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.00, Upana - mita 2.80, Kimo - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO**.
Gari itasafiri muda wa mchana tu (**kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# Viongozi watakiwa kuwafichua wanaojihusisha ndoa jinsia moja

**Na Hamisi Nasri,**
MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni, amewataka viongozi wa dini, kimila na wazee maarufu wilayani humo kuwafichua vijana wanaojihusisha na vitendo vya ushoga na ndoa za jinsia moja ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wito huo ameutoa jana wilayani hapa alipokuwa akizungumza na makundi hayo kwenye kikao maalumu alichokiitisha kujadili namna bora ya kuleta maendeleo kwa njia ya ushirikiano.

Alisema Wilaya ya Masasi ni miongoni mwa zinazotajwa kwa kushamiri vijana wanaojihusisha na vitendo vya ushoga na ndoa za jinsia moja na kwamba kuna haja ya kushirikiana ili kuwafichua wahusika na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kanoni alisema hakuna sheria nchini inayoruhusu vitendo vya ndoa ya jinsia moja pamoja na ushoga na kwamba lazima sheria ichukue mkondo wake ili kukomesha vitendo vya aina hiyo ambavyo kundi kubwa la vijana wanajihusisha.

Alisema serikali wilayani Masasi haitavumilia kuona vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa wakijiingiza kwenye vitendo hivyo ambavyo havikubaliki katika jamii na kutengeneza tabia mbaya kwa kizazi kijacho.

Aliwataka viongozi wa dini, wa kimila na wazee maarufu kushirikiana na serikali ya wilaya kuwafichua vijana wanaojihusisha na vitendo hivyo ili wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ili ichukue hatua.

"Tuwafichue hawa vijana wanaojihusisha na vitendo vya ndoa za jinsia moja na ushoga ili tuwakamate na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria sababu hapa nchini hakuna sheria yoyote inayoruhusu vitendo vya aina hii na havikubaliki kwa jamii yeu," alisema.

Aidha, viongozi wa dini walisema kuwa njia pekee ya kuwafanya vijana waweze kuachana na vitendo visivyo na maadili ni kuwatengenezea mazingira bora ya kiuchumi waweze kujiinua kiuchumi.

Angelusi Mchomanjoma, wa kanisa la Ufufuo Lukuldi Masasi, alisema tatizo kubwa la kupotea kwa maadili hasa kundi la vijana ni kushindwa kufanya kazi na badala yake kutafuta kufanikiwa maisha kwa njia mkato.

Kasimu Mitunda alisema kuwa njia pekee ya kuwafanya vijana kuachana na vitendo vya aina hiyo ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za vitendo hivyo na sio suala pekee la kuichia serikali peke yake.

Alisema vijana wa kikazi hiki wamekosa maadili kutokana na malezi wanayopata tangu wakiwa wadogo mpaka wanakua, kuna haja kwa kila familia kuwa na malezi bora kuwatunza watoto.

Musa Erasto kiongozi wa dini ya kiislamu alisema kuwa serikali inapaswa kuwafanya vijana wafanye kazi za kilimo kwa kuwapa mashamba na kuachana na tabia zisizo na maadili.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumapili tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

MKASA ASKARI-PORI KUDHURU MBARALI...

# Apokwa ng'ombe 170 kinyama, mkazi tangu mwaka 1953 anena

## ●Kiulizo cha mpaka chabaki siri isiyowafikia wanakijiji

**Na Halfani Chusi, aliyekuwa**
MBARALI



Masingija Machiya, mfugaji anayedai kupokwa ng'ombe 170 na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). **PICHA ZOTE: HALFANI CHUSI**



Sepelwa Kashu, miongoni mwa waanzilishi wa Kijiji cha Mwanavala ambacho kina mgogoro wa muda mrefu na TANAPA.

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilianika simulizi ya ukatili dhidi ya wanakijiji wafugaji, ikiendana na dhamira za askari-pori kuwapoka mifugo, udhalilishaji kijinsia wake kwa waume na vipigo.**

**Endelea na hatua zilizofuata, namna kijiji kilivyoanzishwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na ulikojificha utata wa mpaka unaogombewa ambao ndiyo mzizi mkuu wa mgogoro.**

---

Katika ufuatiliaji wake, Nipashe kupitia mwenyeji wake inabaini tukio lingine la mfugaji Masingija Machiya (53) anayedai kuchukuliwa ng'ombe wake 170 na askari wa TANAPA. Anasimulia:

"Mtoto wangu alikwenda kuchunga ng'ombe, huko kambini ambako huwa tunapeleka kwenye eneo la wafugaji Mwanavala. Ilikuwa ni mwezi wa tatu (Machi) mwaka huu, baadaye akanipigia simu kwamba 'baba huku kambini tumeporwa ng'ombe na watu wa hifadhi, walikuja na ndege'".

Anadai kuwa askari hao waliwaswaga ng'ombe kwa kutumia ndege yao, mpaka walipovuka Mto Ruaha wakati mchungaji muda huo wamembana kwenye pori ili asiwazuie.

"Walipomwachia baadaye mwanangu, akaanza kufuatilia kwa nyuma ili kujua wanawapeleka wapi.

"Baada ya taarifa hiyo nimtaarifu mwenyekiti wa kijiji, akamjibu 'mimi siwezi kukusaidia kwa lolote kama walioswaga ni watu wa TANAPA, labda umwambie mtendaji wangu (Ofisa Mtendaji wa Kijiji) maana huyo ndio huwa anawasaidia watu wengi'. Ofisa Mtendaji wa Kijiji ndiye huwa anajua atuandikie nini ndipo twende kugomboa ng'ombe wetu.

"Nikaenda kwa mtendaji, akaniandikia barua, nikaenda Kituo cha Polisi Ubaruku Mbarali kutoa taarifa, wakasema 'sasa sisi unatuambia ili tufanyaje? Sisi hatuwezi kufanya chochote labda tukuandikie tu barua kama ulifikisha malalamiko yako hapa'," anasimulia mfugaji huyo.

Anasema asubuhi ya siku iliyofuata, aliambatana na mjomba wake hadi kambini kwao ili kulipa faini kwa lengo la kupewa ng'ombe wake.

"Tulipofanikiwa kuvuka Mto Ruaha ambako kambi ipo tukabisha hodi, wakatuuliza 'ninyi ni kina nani?' Tukawaambia 'sisi ni wale mlioswaga ng'ombe wetu'. Wakasema 'njooni mnakimbia, hakuna kutembea hapa'.

"Tukaenda huku tunakimbia. Tulipofika cha kwanza wakatuambia 'vueni nguo, toeni mkanda', wakati huo mimi nilikuwa nimechukua fedha Sh. milioni 17 ili kama wakisema faini nilipie maana niliambiwa kila ng'ombe mmoja faini yake laki moja (Sh. 100,000).

"Wakaanza kutupiga kwa saa bili hivi. Baadaye wakatupa adhabu ya kufyeka huku miili yetu ikiwa inauma, mwisho wakaturuhusu na fedha zangu wakachukua kwa nguvu.

"Baada ya kuona imeshindikana nikaenda kwa Mkuu wa Wilaya, akaniambia 'hilo suala lako ni sawa na kumpa nyani kesi ya ngedere kwa sababu hata mimi ninapaswa kuilinda ile hifadhi'," anasimulia mfugaji huyo huku akionyesha majeraha yake yaliyoenea mwili mzima.

Machiya anasema kuwa baada ya hapo, alikwenda Mahakama ya Rujewa, nako akaambiwa kesi yake haiwezi kuisikiliza kwa kuwa hakuwa na ushahidi kama kweli alikuwa na idadi hiyo ya ng'ombe.

Ikisheheni picha pana ya madhira na mgogoro kati ya wanakijiji wa Mwanavala, Kata ya Imalilo Songwe wilayani Mbarali mkoani Mbeya na askari wa hifadhi, Nipashe inatua nyumbani kwa Mzee Sepelwa Kashu, anayejitambulisha yupo hapo kwa miaka 80 sasa kufahamu mzizi wa kijiji, pia msuguano wenyewe.

Mzee Sepelwa, mkazi mwenye asili ya Kimasai, anasema yupo mahali hapo tangu mwaka 1953 na ni miongoni mwa waanzilishi rasmi wa kijiji hicho, akijitambulisha kwamba hata katika kusaidia nchi vita vya Kagera mwaka 1978 alitoa ng'ombe 240, pia anasimulia alijenga shule ya msingi kijijini hapo.

"Wakati wa Mwalimu Nyerere, hiki kijiji kilitaka kufutwa, tukaenda kumwomba akatuambia kama tunaweza kujenga shule atatuuhusu kubaki, ndipo mimi nikaja nikajenga shule hapa, na nikawa ninawalipa walimu mshahara kwa miaka mitatu mpaka pale serikali kuu ilipokuja kunipokea," anaeleza mzee huyo mwenye ng'ombe 12,000.

Mzee Sepelwa aliye mweledi wa eneo hilo, anafafanua historia ya mpaka mahali hapo kwamba bikoni za ardhi zilikuwa jirani na Mto Ruaha, upande wa kijijini kwao, lakini mara zote maelekezo na angalizo walilopewa na serikali ni kutovuka Mto Ruaha.

Anaeleza kuwa bikoni zingine zimewekwa kijijini hapo kwa siri mwaka huu, zinazowatambulisha kuwa wamo ndani ya hifadhi kwa kilomita 10, hatua anayoitaja imechukuliwa bila wao kushirikishwa.

"Kama serikali inalitaka eneo hili, basi itufanyie uthamini mapema, itulipe ili tujue tunakwenda wapi, kwa sababu mkimfukuza mfugaji mwenye ng'ombe wengi bila kumwambia wapi aende, ni sawa na kumfanya afilisike tu," anashauri.

Ni hoja inayopishana na Mkuu wa Wilaya, Kanali Denis Mwila na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Michael Semindu, wanaodai eneo hilo ni batili kwa wakazi kuishi kwa muda mrefu kwa kuwa limekuwa hifadhi tangu mwaka 1910, yaani miaka 51 kabla ya Uhuru wa Tanganyika.

Nipashe ililazimika kupata ufafanuzi wa kisheria na kitaalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, pia ufahamu zaidi kwa aliyekwishaitumikia halmashauri hiyo kwa muda mrefu na sasa yuko katika manispaa mojawapo ya Dar es Salaam (jina tunalihifadhi), ambaye anafafanua:

"Ukiliangalia sakata hili, unaona hao wakazi wanaishi kisheria, lakini kwa sababu serikali inapahitaji, ninadhani ndio maana unaona kuna mgogoro wa mipaka lakini wanaishi nje ya hifadhi tangu enzi za Mwalimu (Julius Nyerere)."

Diwani wa kata hiyo, Chuki Mbwanjine, anakiri kushuhudia mgogoro wa wafugaji na askari-pori. Pia anakiri ng'ombe 170 wa mzee huyo kuchukuliwa na tayari wameshauzwa kwa amri ya mahakama, lakini hajui ni mahakama ipi iliyotoa kibali cha kuuzwa kwa ng'ombe hao.

"Hao ng'ombe bila kuficha wameshaziuzwa. Hawapo! Wanasema wameuzwa kwa amri ya mahakama ya wilaya. Wamiliki walikwenda kuulizia, wakaambiwa hakuna kesi hiyo, wakaambiwa waende Iringa kuna mahakama nyingine ipo huko, nako walijibiwa hivyo hivyo.

"Hili jambo ni baya sana na liko kinyume cha sheria na haki za binadamu, mzee wa watu amekuwa maskini ghafla," alisema diwani huyo huku akionyeshwa kutofurahishwa na tukio hilo.

Anaendelea kueleza kuwa wanakijiji hao wanaishi katika eneo hilo kwa mujibu wa sheria inayowatambua kwamba wapo nje ya hifadhi, lakini mwaka huu walipoweka bikoni nyingine ndipo inawaonyesha wamo ndani ya hifadhi.

"Ukiangalia bikoni ya zamani ambazo ndizo mpaka wa hifadhi na kijiji, zinaonyesha kuwa wapo nje ya hifadhi, lakini kwa mpaka mpya walioweka mwaka huu unaonyesha wamo ndani, na kibaya zaidi walikuja na askari siku wanapoweka bikoni nyingine hata wananchi walikosa muda wa kuchangia hoja," anaeleza.

Kuhusu wanakijiji walioteswa na askari wa TANAPA, kiongozi huyo anakiri kushuhudia na kuthibitisha kuwa aliwakuta katika eneo walikokumbana na mateso dakika chache baada ya kupewa taarifa. Aliwakuta wakiwa hawana nguo huku miili yao ikiwa na mabaka ya kuunguzwa kwa moto.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Imalilo Songwe, Angelina Mtweve, anakiri kuwa kata yake ina mgogoro wa muda mrefu kati ya wanakijiji na hifadhi, jambo ambalo huzua taharuki mara kwa mara na kusababisha majeruhi.

Anashauri uthamini ufanyike haraka ili wanakijiji walipe stahiki zao, wasiendelee kunyanyasika, pia akisoa mateso dhidi yao. Hata kama wamekosa, wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Kuhusu aliyepokwa ng'ombe wake na TANAPA, Angelina anasema "...na mimi nimesikia siku Mkuu Wilaya alipoenda kuongea na wafugaji ndipo huyo mzee alitoa malalamiko yake kisha akaambiwa aende ofisini kwake na taarifa zake ili apatiwe msaada.

"Na waliodai kuteswa wakiwa uchi hilo ni kweli, na tulipokwenda hata siku ile baada ya kupewa taarifa tulifika mahali ambako nguo walizokuwa wamevaa zilichomwa moto, mpaka leo ninadhani ushahidi haujafutika."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwanavala, Chesco Kapunga, anasema kilisajiliwa kama kijiji cha wafugaji na hata waliokutwa na askari wa TANAPA walikuwa kwenye maeneo yao halali kisheria.

Kapunga pia anathibitisha kuwapo migogoro kati ya wafugaji, wakulima na askari wa TANAPA, pia kuwapo matukio ya wanakijiji kuvuliwa nguo na kuunguzwa kwa mapanga na mifugo yao kutaifishwa. Si taarifa mpya za matukio ofisini kwake.

"Kwa mfano, yule mzee alikuwa na ng'ombe wengi sana (170), sasa hivi amebaki maskini anahangaika, hana chochote, ana wake wanne na watoto 24. Watoto watatu wameacha shule kwa sababu hana uwezo tena wa kusomesha," anaeleza.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mapinduzi, ambako tukio lilitokea, Yasaire Kimosa, anaungana na mwenyekiti wa kijiji chake, akisema kitongoji chake kipo nje ya hifadhi tangu enzi za Mwalimu, japo anashanga kuona ghafla serikali inasema wamo ndani ya hifadhi.

Kuhusu walioteswa wakiwa uchi na kifo cha kijana aliyeuawa na askari, Kimosa anakiri kuwa na taarifa za matukio hayo. Alikuwa miongoni mwa mashuhuda na waliwakuta wanakijiji wenzao wakiwa hawana nguo.

## Kiwanda kuchakata tani 12 mihogo mibichi kujengwa

**Na Christina Mwakangale,** IRINGA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), imesema inajenga kiwanda cha kuchakata tani 12 kila siku za mihogo mibichi, kitakachojengwa kijiji cha Kwa Chaga, Mkata, Handeni mkoani Tanga na kunufaisha wakulima 6,000 wa eneo hilo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CPB, John Maige, aliyasema hayo jana, mkoani Iringa, wakati wa kikao kazi baina ya bodi hiyo na wahariri na waandishi wa habari kutoka vyombo vya habari nchini.

Maige alisema, hadi sasa kiwanda hicho kimegharimu Sh. milioni 350 na kitaanza kufanya kazi mapema mwezi Julai, mwaka huu, huku wanufaika wakiwa wakazi wa eneo hilo, ambalo litatoa ajira zisizo rasmi 80 na rasmi tano.

"Handeni tumebaini ni miongoni mwa maeneo yanayoongoza katika kilimo cha mizizi, yaani mihogo ikilinganishwa na maeneo mengine 25 ambayo tutayafikia kwa kuwa na viwanda vya uchakataji kama hiki, ikiwamo mkoani Mtwara, Kigoma na Mkuranga (Mkoa wa Pwani)," alisema Maige.

Alibainisha teknolojia inayotumiwa na CPB ni ya kisasa inayochakata mazao kwa muda mfupi na kupakiwa na kuwa tayari kwa matumizi, ikiwamo unga wa ngano, muhogo na mahindi kwa kutoa aina ya sembe na dona.

"Tunahamasisha Watanzania kutumia fursa ya soko la nje, lakini hata wakulima wa ndani tunanunua mazao yao, tunawafikia kupitia vikundi vya wakulima, AMCOS, wakulima wao wenyewe na kununua mazao yaliyo chini ya bodi.

"Mazao hayo tukinunua tunayongezea thamani, kuyauza ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo CPB inampa uhakika wa soko mkulima na muuzaji wa mazao, pia anapata fursa ya kutumia miundombinu ya CPB, yaani maghala, kusagisha, kukausha kwa gharama nafuu," aliongeza Maige.

Alisema nchi za Kenya na Rwanda zimeingia makubaliano na CPB, ili kuwauzia mazao ya nafaka hasa mahindi na zao jamii ya kunde hususan maharage mekundu yanayohitajika zaidi nchi jirani.

"Tunasimamia mazao aina tofauti ikiwamo, mahindi, mbaazi, karanga, korosho ufuta, mawese, alizeti, mchele, ngano na mengine ambayo tunayachakata baadhi kuwa unga, siagi," alisema Kaimu Mkurugenzi huyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Biashara CPB, Evans Mwanibingo, alisema CPB ina maghala ya aina tofauti ikiwamo vihenge, kwa kuhifadhi tani 112,000 kwa mwaka, kwenye ghala za kikanda za Bodi hiyo, zilizopo mikoa mitano, Iringa, Arusha, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

Aliongeza kwamba Shirika la Chakula Duniani (WFP), limeomba kutumia kati ya ghala hizo kuhifadhi tani 15,000 huku Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), ikiomba kupatiwa ghala pia, ili kutunza mazao ya nafaka zinazozalisha bidhaa za kampuni hiyo.

# Kundi la wanaume kufikiriwa mikopo ya makundi maalum

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inaangalia uwezekano wa kuweka kundi la wanaume katika mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri ili kuwainua kiuchumi.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas.

Katika maswali yake, mbunge huyo alihoji kwa kuwa serikali ipo katika maboresho ya utoaji wa mikopo ya asilimia 10, haioni ni muda sahihi wa kufanyia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa ili kuongeza kundi la wanaume katika utoaji wa mikopo hiyo.

"Serikali haioni kuwa kutomweka mwanamume katika mikopo hiyo kunamrudisha nyuma, kumbagua na kuondoa umoja katika familia kwa kuwa katika jamii nyingi za Tanzania mwanamume ni kiongozi wa familia," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Ndejembi alisema kwa sasa serikali inafanya mapitio ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ili iboreshwe na iendane na wakati.

Alisema timu ya wajumbe iliyoteuliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Kairuki, imeshaanza kufanya kazi ya mapitio ya sera hiyo na moja kati ya mambo watakayo yaangalia ni namna ya kuingiza kundi hilo katika mikopo hiyo.

"Na hili la pili la kuona wanamume ni namna gani wanaingizwa kwenye unufaikaji wa mikopo hii, Mheshimiwa Naibu Spika, tayari timu hii itaangalia pia uwezekano wa hili, lakini katika makundi haya wanaume wapo katika makundi ya vijana, wanamume wapo kwenye makundi ya walemavu," alisema Ndejembi.

Alisema, timu hiyo itakapomaliza kazi ya kufanya mapitio ya sera hiyo muswada utawasilishwa bungeni kupitia Kamati ya Bunge ya Kudumu kwa ajili ya kujadiliwa kisha kufanyiwa marekebisho.

Awali, katika swali lake la msingi, Mbunge huyo alihoji ni kwanini serikali isiongeze kundi la wanamume kwa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Naibu waziri huyo alijibu kwa sasa mikopo ya asilimia 10 inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 Kifungu cha 37A ya mwaka 2018 na Kanuni za Usimamizi na Utoaji wa Mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019 na kanuni za marekebisho za mwaka 2021.

Alisema mikopo hiyo inatolewa kwa ajili ya kuwezesha makundi hayo kupata mikopo isiyo na riba kwa kuzingatia hayawezi kupata mikopo katika taasisi zingine za fedha kwa sababu ya kukosa dhamana na uwezo mdogo wa kumudu riba ili kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kujiongezea kipato.

"Serikali itaendelea kusimamia utoaji wa mikopo hii kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Aidha, makundi mengine ambayo sio walengwa wa mikopo hii wanashauriwa kupata kupitia taasisi zingine za fedha zinazohusika na utoaji wa mikopo hiyo," alisema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza wakati wa ufunguzi wa kambi ya mafunzo ya biashara changa za vijana 196 (startups) zilizoingia katika hatua ya awali kabla ya kupewa mitaji wezeshi kwa ajili ya kuendeleza biashara zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Majaliwa atoa maelekezo maalum udhibiti wa kelele

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaelekeza wakuu wa mikoa yote ya Tanzania Bara wakae na Mabaraza ya Biashara na wamiliki wa kumbi za starehe katika mikoa yao kwa madhumuni ya kutafuta mwafaka wa pamoja katika utekelezaji wa sheria, kanuni na mwongozo kuhusu udhibiti wa athari zitokanazo na sauti zilizozidhi viwango.

Pia amezielekeza Idara za Mipangomiji katika halmashauri za wilaya zote nchini zitenge maeneo ya ujenzi wa nyumba za ibada kama wanavyotenga maeneo ya taasisi nyingine.

Alielekeza hayo jana alipozindua Kongamano la Kujengewa Uelewa kuhusu madhara yatokanayo na sauti zilizozidi viwango katika nyumba za ibada. Kongamano hilo lililoandaliwa na Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alisema ipo miongozo inayosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inayohusu masuala ya usimamizi wa mipango miji.

"Ninasisitiza toeni miongozo mahsusi ya mipango ya matumizi ya ardhi. Kwa upande wa udhibiti wa sauti zilizozidi, kila mamlaka iliyotoa vibali au leseni ya shughuli au biashara, zifuatilie mwenendo wa matumizi ya leseni hizo.

"Ninasisitiza kuwa kila mamlaka itimize wajibu wake kulingana na maelekezo yaliyomo katika Mwongozo wa Uthibiti wa Uchafuzi wa Mazingira Utokanao na Kelele na Mitetemo uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

"Leo (jana) kuna kongamano la kitaifa linaloratibiwa na JMAT, NEMC wekeni mpango wa kufanya makongamano kama haya hadi katika ngazi ya mikoa ili jamii iwe na uelewa wa pamoja kuhusu athari za viwango vya sauti vinavyozidi. Pia, toeni elimu kwa umma ili wajue viwango halisi vya sauti vinavyostahili wakati wa mchana na wakati wa usiku."

Akizungumzia kuhusu wamiliki wa majengo, Waziri Mkuu aliwataka wafanye tathmini ya athari ya mazingira kwa watu wanaotumia majengo hayo pamoja na wakazi wa jirani na majengo hayo kwa lengo la kubaini madhara kwa watumiaji wa majengo hayo na jamii inayozunguka.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwasisitiza viongozi wa dini na washiriki katika kongamano hilo waendelee kuwa vielelezo na mabalozi wazuri wa kufikisha yale mambo mazuri yanayowasilishwa katika kongamano hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema madhumuni ya kongamano hilo ni kuwakutanisha pamoja viongozi wa dini na mila ili kutoa elimu ya athari za sauti zilizozidi viwango kutoka katika nyumba za ibada na jamii.

Alisema kanuni za udhibiti wa kelele na mitetemo za mwaka 2015 zimeainisha viwango vinavyoruhusiwa katika maeneo ya makazi, nyumba za ibada, biashara, viwanda na hospitali kwa ajili ya jamii, akitolea mfano viwango vya sauti vinavyoruhusiwa katika nyumba za ibada zilizopo maeneo ya makazi ni dBA 60 wakati wa mchana na usiku dBA 40.

Alisema sauti zinazozidi viwango katika nyumba za ibada zinaweza kuathiri afya za waumini waliopo katika nyumba za ibada na maeneo ya jirani na kusababisha matatizo ya kusikia, usingizi na kuathiri uwezo wa kufanya kazi pamoja na kusababisha migogoro kati ya wakazi na viongozi au waumini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matapeli wasigeuze vitambulisho vya NIDA mradi

**KUMEKUWA** na tabia ya baadhi ya watu wanapotakiwa kufanya jambo fulani kwa faida yao ya baadaye inawachukua muda mrefu kulitekeleza.

Mfano halisi ni suala hili la Vitambulisho vya Taifa ambavyo vinatolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Wakati mchakato wa kuvipata vitambulisho hivyo ulipoanza, mamlaka hiyo ilijitahidi kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe faida ya kuwa na vitambulisho hivyo.

Hata hivyo, baadhi ya watu ambao wengi wao kwa sasa wanahaha kuvipata, hawakulichukulia maanani.

Wengi wanahangaika kuvipata baada ya kupata safari au wanapotaka huduma muhimu na kutakiwa kuonyesha vitambulisho hivyo, ndipo huanza kuhangaika huku na kule kuvipata.

Kuna watu ambao wanatumia fursa hiyo ya watu kuhangaika kuwatapeli kwa kuwadanganya kuwa watawapatia kwa urahisi.

Wengine wameshatapeliwa pesa nyingi, bila kupata vitambulisho hivyo, kwa sababu ni lazima mhusika anayekitaka afuate mchakato unaotakiwa na mamlaka hiyo ikiwamo kujibu maswali muhimu.

Hiyo inasaidia kuepusha vitambulisho hivyo kuwafikia watu wasio raia wa Tanzania.

Mfano mzuri ni tukio lililotokea hivi karibuni la vijana waliochaguliwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kutakiwa kuwa na vitambulisho hivyo.

Kutokana na hali hiyo, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, imewataka Watanzania wenye vigezo ikiwamo waliotimiza umri wa miaka 18 kufuatilia vitambulisho vya taifa mapema badala ya kusubiria matukio yanayohitaji vitambulisho hivyo.

Maelfu ya vijana walifurika kwenye ofisi zake zilizo katika wilaya mbalimbali wakihitaji Vitambulisho vya Taifa baada ya kuitwa kujiunga na JKT.

Hali hiyo inaleta usumbufu mkubwa na kuleta mkwamo kwa kundi hilo kujipatia vitambulisho huku wengine wakiripotiwa kutapeliwa na watu waliowaahidi kuwapatia vitambulisho kwa haraka.

Pia mamlaka hiyo imesema kuna njia nyingine ambayo wananchi wanaweza kuitumia na wakapata vitambulisho bila usumbufu.

Wananchi wanaomudu kutumia mtandao wanaweza kujisajili kupitia njia hiyo, kitu cha msingi ni kuweka taarifa zako ambazo zitarahisisha mchakato wa kupata kitambulisho cha NIDA bila usumbufu wowote.


Mamlaka hiyo imekuwa ikiwasisitiza watu wafuatilie vitambulisho mapema badala ya kusubiri matukio maalumu. "Kwa mfano Juni 5, mwaka huu ilisambaa taarifa kwa umma ambayo inawaita wahitimu wa kidato cha sita, hao wanaokwenda JKT kujitokeza kuweka sawa taarifa zao ili wapate vitambulisho kwa urahisi, lakini wakati huo huo, watu wasio na nia njema nao wakatumia nafasi hiyo wakawa wanawarubuni kwamba watawasaidia kupata vitambulisho hivyo kwa haraka," hii sio sawa tunatakiwa kuchukua tahadhari." Mamlaka hiyo ilifafanua.

Tabia ya kupata huduma kwa mtindo wa zimamoto, sio tu unasumbua mtu anayetaka huduma hiyo, bali hata watumishi wa ofisi hizo ambao ina walazimu kufanya kazi kwa muda wa ziada kuwahudumia.

Mamlaka hiyo ilitoa mfano katika Wilaya ya Ilala pekee walipokea vijana 200 hadi 250 kwa siku waliokuwa wanahitaji vitambulisho hivyo.

Watanzania tubadilike, tuwe na kawaida ya kufanya mambo yetu kwa wakati ili kuepusha usumbufu kama huu unaojitokeza wakati mtu anapotakiwa kuwa na kitambulisho na kutokuwa nacho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Wanafunzi vijiwe vituo vya daladala wafuatiliwe

**BAADHI** ya madereva na makondakta wa daladala hasa majijini na mijini, wamekuwa wakilalamikiwa kwa kuacha wanafunzi vituoni, kitendo ambacho kinasababisha washindwe kuwahi kufika shuleni kwa wakati, lakini wakwame kurejea nyumbani wengine wakifika hata baada ya saa 2:30 usiku.

Ikumbukwe wakichelewa kufika nyumbani, hukosa muda wa kujisomea na kupumzika lakini hata kuwasaidia wazazi na walezi wao shughuli za nyumba kwa vile haiwezekani mwanafunzi kwenda shule pekee bila hata kusaidia kuosha vyombo jikoni.

Ni kweli matukio hayo yamekuwa wakitokea kila mara. Kwa wale wanaotumia usafiri huo, hasa jijini Dar es Salaam, watakuwa wamewahi kushuhudia jinsi wanafunzi wanavyoachwa vituoni muda wa asubuhi na jioni kukiwa kuna abiria wengi vituoni.

Daladala zinaelekezwa kubeba wanafunzi watano kila moja ili kuhakikisha wanawahi vipindi vya masomo au kurudi nyumbani kwa wakati, lakini hilo limekuwa likifanyika kwa mvutano na kauli kuwa hili siyo darasa zinatamalaki muda wote. Wakati hali ikiwa hivyo, ipo pia haja ya kuangalia upande wa pili wa shilingi, kwani wapo baadhi ya wanafunzi ambao hukaa vituoni muda mrefu hata kama wakiitwa kupanda daladala hawataki ili mradi wajicheleweshe kwa kisingizio cha kukosa usafiri.

Inawezekana wanatumia kisingizio cha kutoruhusiwa kupanda daladala, ili wafanye mambo yao mitaani. Hivyo ungefanyika msako katika vituo hivyo ili kuwabaini na kuwachukulia hatua.

Wapo baadhi yao hadi saa 2:00 asubuhi wapo katika vituo vya daladala wakiendelea na mazungumzo kana kwamba hawaendi shule au muda wa vipindi vya masomo bado.

Mfano mmojawapo ni kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, si ajabu kukuta wanafunzi wamekaa wanaendelea na mambo yao hata baada ya muda wa masomo kuanza na wengine hata saa 12 jioni hata kama wanaitwa kupata daladala hawaendi.

Hivyo, wakati umefika tena kuna haja wazazi na walezi kuwafuatilia wanafunzi hao, ili kujua kama wanafika shuleni kama wanavyoaga nyumbani isijekuwa wanatumia kisingizio cha kukataliwa na daladala, kumbe wana mambo yao.

Njia hiyo inaweza kumaliza mzizi wa fitina, hasa ule wa kudai kwamba wanakataliwa kupanda daladala na kumbe wana mambo yao ambayo mwisho wake si mzuri kwa maendeleo ya elimu.

Wakati wakifanya hayo, vipo baadhi ya vituo vya daladala ambavyo makondakta na madereva wakiwaona wanarandaranda, huwa wanawalazimisha kupanda daladala waende shule au nyumbani.

Miongoni mwa vituo hivyo ni Makumbusho, ambako madereva na makondakta waliopata elimu kupambana na ukatili wa kijinsia, hufanya kazi hiyo wanapowaona wanafunzi wenye mtindo huo.

Hao ni wale waliopata mafunzo kutoka Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), ambalo linafanya kampeni ya kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi, wasichana na wanawake.

Kupitia mafunzo hayo ya WAJIKI baadhi ya madereva na makondakta wa daladala wamekuwa ni mabalozi wa kuyaeneza kwa wenzao, huku wakihakikisha hakuna wanafunzi wanaorandaranda vituoni.

Ingekuwa ni vyema kama mafunzo hayo yatasambaa kwa makondakta na madereva wa vituo vyote vya daladala, jijini Dar es Salaam, ili kusaidia kuwaepusha wanafunzi kujiingiza katika makundi mabaya.

Kwa sasa imekuwa ni kawaida kukuta wanafunzi wa aina hiyo wamevaa suruali mlegezo, kitambaa kikining'inia katika mfuko wa nyuma wa suruali ambazo zibanwa chini.

Ukweli unabaki kuwa wapo wanaowazuia wanafunzi kupanda daladala lakini pia kuna wale wasiopanda daladala kwa sababu wanazozijua wenyewe na kubaki wakirandaranda vituoni, na hao huenda wanajihusisha na uhalifu hivyo, wazazi, walezi, polisi na jamii isiwafumbie macho iwafuatilie.

# Mbunge apigania ujira madereva IT

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, amehoji lini serikali itashughulikia kuboresha ujira wa madereva wa magari ya IT ambao hulipwa kilometa 900 kwa Sh. 100,000.

Akiuliza maswali bungeni jana, Mbunge huyo alisema kuna haja ya serikali kutoa tamko ili waajiri wa madereva wafuate amri ya kima cha chini cha mshahara kupata mikataba halali itakayowapatia ujira badala ya kilometa 900 kulipwa Sh. 100,000.

"Kwa kuwa utaratibu unaonesha dereva wa IT haruhusiwi kuwa na msaidizi, tukumbuke magari haya yanakwenda kilomita nyingi zaidi ya 900, kuna haja ya serikali kuwa na wasaidizi ili wapunguze ajali kwa kuwa magari yao yanapata ajali sana kutokana na uchovu," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema utaratibu wa kazi kwa madereva wanaoendesha magari ya IT unafanyika kwa kuingia makubaliano ya kazi kati ya mmiliki wa gari na dereva husika na malipo hufanyika baada ya mhusika kufikisha gari linapokwenda.

Alisema madereva hao wanafanya makubaliano ya mdomo na serikali imekuwa ikishauri yafanyike kwa maandishi ili kulinda stahiki zao.

Katambi alisema serikali kwa kutambua mchango wa sekta mbalimbali katika uchumi ikiwamo sekta ya usafirishaji, imepanga kima cha chini cha mshahara kilichoboreshwa ambacho kimeanza kutumika Januari mosi, mwaka huu.

Alitoa rai kwa madereva wa magari ya IT kuingia mikataba ya kazi ya kibiashara na atakapotokea mwajiri au kampuni ambayo itaajiri madereva kwa ajili ya kuendesha magari ya IT, atapaswa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ambayo inaelekeza ulipaji wa ujira kulingana na sekta hiyo.

**"Kwa kuwa utaratibu unaonesha dereva wa IT haruhusiwi kuwa na msaidizi, tukumbuke magari haya yanakwenda kilomita nyingi zaidi ya 900, kuna haja ya serikali kuwa na wasaidizi ili wapunguze ajali kwa kuwa magari yao yanapata ajali sana kutokana na uchovu," alihoji.**



Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Patrick Ole Sosopi, akihutubia mkutano wa hadhara katika Kata ya Mbolimboli Jimbo la Isimani mkoani Itinga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIDA yatoa njia mbadala kurahisisha kupata vitambulisho

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imewataka Watanzania wenye vigezo ikiwamo waliotimiza umri wa miaka 18 kufuatilia Vitambulisho vya Taifa mapema badala ya kusubiri matukio yanayohitaji vitambulisho hivyo.

NIDA imetoa kauli hiyo ikiwa ni siku chache baada ya maelfu ya vijana kufurika kwenye ofisi zake katika wilaya mbalimbali wakihitaji vitambulisho hivyo baada ya kuitwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Msemaji wa NIDA, Geofrey Tengeneza, alisema mafuriko hayo ya vijana yaliyojitokeza hivi karibuni, yameripotiwa kusababisha usumbufu na kuleta mkwamo kwa kundi hilo kupata vitambulisho huku wengine wakiripotiwa kutapeliwa na watu waliowaahidi kuwapatia kwa haraka.

Tengeneza alisema ipo njia nyingine ambayo wananchi wanaweza kuitumia na wakapata vitambulisho bila usumbufu kwa kutumia mtandao kujisajili.

"Wananchi wanaomudu kutumia mtandao wanaweza kujisajili, kitu cha msingi ni kuweka taarifa zako ambazo zitarahisisha mchakato wa kupata kitambulisho cha NIDA na hakuna usumbufu," alisema Tengeneza.

"Tumekuwa tukisisitiza watu wafuatilie vitambulisho mapema badala ya kusubiri matukio maalumu. Kwa mfano Juni 5, mwaka huu, ilisambaa taarifa kwa umma ambayo inawaita wahitimu wa kidato cha sita, hao wanaokwenda JKT kujitokeza kuweka sawa taarifa zao ili wapate vitambulisho kwa urahisi, lakini wakati huo huo watu wasio na nia njema nao wakatumia nafasi hiyo kuwarubuni kwamba watawasaidia kupata vitambulisho hivyo kwa haraka, hii sio sawa tunatakiwa kuchukua tahadhari," alisema.

Tengeneza alisema kutokana na vijana kufurika wakihitaji vitambulisho hivyo, watumishi wa ofisi hizo walilazimika kufanya kazi kwa muda wa ziada kuwahudumia na kwa Wilaya ya Ilala pekee walipokea vijana 200 hadi 250 kwa siku waliokuwa wanahitaji vitambulisho hivyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Nyama ya Tanzania kuanza kuuzwa Misri

**Na Mbaraka Kambona**

NYAMA ya Tanzania itaanza kuuzwa nchini Misri baada ya ujumbe kutoka nchini humo kukutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega na kumweleza kuwa lengo lao kabla ya Sikukuu ya Eid al Hajj waanze kusafirisha tani 100 za nyama ili kuanza kutangaza soko la Tanzania.

Hayo yalifahamika wakati wa kikao cha "Breakfast Meeting" kilichofanyika jijini Dodoma jana baina ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Ujumbe kutoka nchini Misri ulioongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Taifa ya Huduma za Miradi (NSPO), Meja Jenerali Hossam Nigeda.

Meja Generali, Nigeda alimweleza Waziri Ulega kuwa lengo lao ni kuendelea kuimarisha ushirikiano wa nchi hizo mbili kwa kufungua soko la nyama ya Tanzania nchini Misri.

Pia wamejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa hapa nchini ambayo itawawezesha kusafirisha tani 600 ya nyama kila mwezi, kusafirisha wanyama hai wakiwamo ng'ombe, kondoo na mbuzi 10,000 kila mwezi.

Alifafanua kuwa kwa siku za hivi karibuni wapo katika mipango ya kusafirisha tani 100 za nyama kabla ya Sikukuu ya Eid Al Hajj ili kuanza kutangaza soko la nyama ya Tanzania nchini humo.

Misri ni miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya watu barani Afrika ambao hawapungui milioni 120 na kuwa fursa nzuri ya kibiashara kwa Tanzania hususani biashara ya nyama.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ulega alimhakikishia Meja Jenerali Nigeda kuwa Tanzania ipo tayari na watawapa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha biashara hiyo iweze kuanza haraka iwezekanavyo.

Wajumbe wengine waliombatana na Meja Jenerali Nigeda ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji, Islam Attia Abdel Hamid, Mwenyekiti wa Huduma za Mifugo, Misri, Meja Jenerali, Dk. Ihab Saber Youssef na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Masr Trading, Dk. Hatem Ahmed.

Ziara hiyo ni miongoni mwa jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kufungua milango ya kibiashara nje ya nchi.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization (HDO), Prisca Ngweshemi, akitoa mafunzo ya malezi kwa baadhi ya wazazi na walezi wa Kata ya Kitunda jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni mwendelezo wa shirika hilo wa kutaka kurejesha maadili mema katika jamii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali kusaini mkataba TRA kupata taarifa nchi 146 duniani

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI inatarajia kusaini mkataba utakaowezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupata taarifa mbalimbali kutoka katika nchi 146 duniani ambazo zitasaidia kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa miamala ya kimataifa.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina.

Mbunge huyo alihoji kwa kiwango gani serikali imejiimarisha kukagua miamala ya uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa na huduma baina ya kampuni ya kimataifa.

Akijibu swali hilo, Chande alisema kwa kuzingatia vihatarishi vilivyopo kwenye miamala husika, serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha udhibiti na kuzuia upotevu wa mapato.

Alitaja hatua hizo ni pamoja na kuanzisha Kitengo Maalum cha Usimamizi wa Kodi za Kimataifa ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzia 2011, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa kanuni na miongozo kuhusu ukaguzi wa kodi kwenye kampuni zenye mahusiano.

"TRA imenunua Kanzidata ya Orbis kwa ajili ya kupata taarifa za kusaidia kufananisha bei za miamala ya kimataifa ili zisaidie kujenga hoja wakati wa ukaguzi unaofanywa kwenye kampuni za hapa nchini," alisema.

Aidha, alisema Tanzania imejiunga na Jukwaa la Kimataifa la Ubadilishaji wa Taarifa za Kikodi kwa lengo la kuhakikisha nchi inajenga uwezo wa kubadilishana taarifa za kikodi na nchi nyingine.

Katika maswali yake ya nyongeza, Mbunge huyo alihoji hatua hizo zimesaidia kwa kiwango gani kuongeza mapato na kuhoji serikali inatoa kauli gani kuhusu ongezeko kubwa la taarifa shuku za fedha haramu.

"Miamala ya usafirishaji fedha imeongezeka kutoka Sh.trilioni 123 hadi Sh.trilioni 280 mwaka 2023, ishara hii inaonesha ongezeko kubwa la rushwa, ufisadi, serikali inatoa kauli gani,"alihoji.

Akiongezea majibu ya maswali hayo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, alisema kwa mujibu wa sheria ya utakatishaji fedha taarifa shuku zilizowasilishwa zinaendelea kufanyiwa kazi na vyombo vya sheria.

# Viongozi sekta ujenzi watakiwa kubuni mbinu za kiutendaji

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJIMENTI ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) pamoja na taasisi zake wametakiwa kubuni mbinu za kiutendaji zinazolenga kuweka mazingira wezeshi yenye kuchochea na kuimarisha ari na morali kwa watumishi wanaowasimamia.

Wito huo ulitolewa mkoani Tanga na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, wakati akifungua kikao kazi kati ya menejimenti ya sekta hiyo pamoja na menejimenti za taasisi zake ambazo ni TANROADS, TBA, TEMESA, RFB, ERB, CRB, AQRB, NCC, ICoT na vikosi vya ujenzi.

Alisisitiza kwa viongozi na watendaji hao kuwa huru kuelezana ukweli kuhusu masuala yanayohusu utendaji wa kisekta na kuleta mabadiliko ambayo yataongeza tija na uzalishaji katika sekta hiyo.

"Kikao hiki madhumuni yake ni kuandaa mikakati na kupanga namna ya kuongeza ari na morali kwa watumishi kwa kuelezana ukweli na kutafuta majibu ya changamoto za watumishi kila kiongozi katika maeneo yao ya kazi," alisisitiza Prof. Mbarawa.

Alisema suala la morali kwa watumishi ni muhimu likapewa kipaumbele kwasababu morali ni kichocheo muhimu katika utendaji kazi.

"Morali ya watumishi ikiwa juu hapana shaka watajituma bila kusukumwa na kusaidia menejimenti zenu kuwasimamia kwa unafuu mkubwa," alisema.

Akitaja mafanikio yaliyofikiwa na sekta hiyo, Prof. Mbarawa alisema TANROADS imekwisha tekeleza ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 1,151.37 kwa kiwango cha lami na barabara zenye urefu wa kilomita 4, 140.76 zimefanyiwa upembuzi yakinifu.

Miradi mingine ni ujenzi wa madaraja makubwa nane na madaraja mengine sita yameshafanyiwa upembuzi yakinifu pamoja na uboreshaji wa viwanja vya ndege 19 vilivyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mafanikio mengine ni upande wa TBA imetekeleza ujenzi wa nyumba za watumishi 150 kwa awamu ya kwanza, ujenzi wa nyumba 20 za viongozi zikiwa katika hatua mbalimbali na ujenzi wa nyumba za majaji katika mikoa mbalimbali.

Pia ujenzi wa vihenge vya kisasa na maghala ya kuhifadhia chakula katika mikoa minane nchini, usimamizi wa ujenzi wa majengo 17 na jengo moja la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama mkandarasi.

Kadhalika, ujenzi wa vivuko vipya, ukarabati wa vivuko, ujenzi wa maegesho na miundombinu ya vivuko, ujenzi wa karakana mpya na vilevile mikataba ya ununuzi na usimikaji wa mifumo ya kielektroniki ambayo yote yatasaidia kutatua changamoto za miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Katibu Mkuu wa Sekta ya Ujenzi, Balozi Aisha Amour, alisema kuwa katika kikao hicho watabadilishana maarifa na uzoefu miongoni mwa watendaji wakuu wa wizara na taasisi zake.



## Prof. Mbarawa ataja faida uwekezaji Bandari Dar es Salaam

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema uwekezaji ambao serikali imeingia ubia na Kampuni ya DP World ya Dubai, una maslahi mapana kwa nchi.

Amesema maslahi hayo ni pamoja na kuchangia kuiwezesha bandari kuongeza mapato kwa nchi, kutoka asilimia 37 hadi kufikia asilimia 67.

Mbarawa aliyasema hayo jana jijini Tanga, wakati akifungua kikao kazi kati ya menejimenti ya wizara hiyo na menejimenti za taasisi zake.

Waziri Mbarawa, alisema mkakati wa serikali ni kuifanya Bandari ya Dar es Salaam ifanye kazi kwa ufanisi na mkakati mojawapo ni kuwapelekea kwenye viwango vya kimataifa ili waweze kushirikiana na TPA ili kuweza kuboresha bandari zao.

Aidha, alisema mwekezaji huyo ana viwango vya kimataifa vya kuiwezesha TPA kuboresha bandari kutokana na kwamba ni kampuni kubwa kati ya kampuni 10 duniani zinazofanya mambo hayo.

Alizitaja kampuni nyingine ni Singapore Ports Authority, Harshon ya Honkong na MPM.

Alisema wameamua kuchukua kampuni hiyo baada ya kufanya uchambuzi wa kina kwa sababu wana sifa za kipekee ukilinganisha na wengine.

Alitaja sifa zake kuwa pamoja na kufanya kazi kwenye bandari sita Afrika, ikiwamo kufanya kazi na bandari 30 ulimwenguni kote, lakini wanameli zaidi ya 100 za kuchukulia mzigo duniani.

Vilevile, alisema kwamba Kampuni ya DP Word wana uwezo wa meli nyingine za kuchukulia watalii, kuhamasisha mnyororo mzima wa mizigo toka unapotoka mpaka unafika kwa mteja wa mwisho ikiwamo uwezo wa kujenga bandari kavu maeneo mbalimbali.

# Mfanyabiashara adaiwa kumpiga risasi mkulima

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

JESHI la Polisi mkoani Manyara limemtia mbaroni Paulo Sipiteki (43), mfanyabiashara wa mifugo na mkazi wa Arusha, aliyekuwa amekimbilia mafichoni baada ya kudaiwa kumpiga risasi begani na kumjeruhi mkulima mmoja mkazi wa Simanjiro.

Mfanyabiashara huyo alimpiga risasi, Walter Kaaya (34) baada ya kuibuka mzozo wa ng'ombe wake kuvamia shamba la mkulima huyo lenye ukubwa wa ekari 200 likiwa na mazao ya mahindi na maharage.

Jana Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, alithibitisha kukamatwa kwa Sipiteki, aliyekuwa ametoroka kukwepa mkono wa dola tangu Mei 24, mwaka huu.

"Askari kanzu wetu walimkamata mtuhumiwa huyo, akiwa amejificha huko katika Kijiji cha Nyumba ya Mungu, Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro. Alifanya hivyo kwa sababu ya kiburi cha mali na silaha alizonayo, ndio ilimfanya atumie nguvu.

"Wananchi walifikiri kwamba mtuhumiwa ni mtu mwenye mifugo mingi na fedha, kwa hiyo ni vigumu kukamatika. Lakini sisi polisi kwa weledi wetu na maadili, tumemtia mbaroni na sasa tunafanya utaratibu wa kumfikisha mahakamani," alisema.

Kuhusu hali ya majeruhi huyo, Katabazi, alisema Walter Kaaya, kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC iliyoko Moshi, mkoani Kilimanjaro akiendelea kupatiwa matibabu.

"Kosa kubwa hapo ni kujeruhi, hasa ikizingatiwa mahali alipojeruhiwa Kaaya, mtu anaweza kupoteza maisha. Tunashukuru Mungu anaendelea vizuri na matibabu KCMC, maana kabla hatujaangalia uharibifu wa mazao, uhai wa binadamu unapewa kipaumbele," alieleza Kamanda Katabanzi.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera (katikati), wakitembelea Kijiji cha Kimotorok, Kata ya Loiborsiret kwenye mgogoro wa mpaka wa kijiji hicho na Pori la Akiba la Mkungunero juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Uongozi wa shule wadaiwa kumpoka kifaa mwanafunzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANAFUNZI wa Shule ya Msingi Nshupu, Kata ya Nkwaranga, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Samweli Apael (16), ameulalamikia uongozi wa shule hiyo 'kupoka' kifaa chake maalum kinachomwezesha kuandika na kusomea kutokana na ulemavu wa mikono alionao.

Samweli, alipewa mwaka jana kifaa hicho, aina ya ipad na mhisani mmoja aliyeguswa na ulemavu alionao.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu magumu anayopitia, mwanafnzi huyo alisema hivi sasa anapata wakati mgumu kwenye masomo yake baada ya uongozi wa shule hiyo kubinafsisha kifaa chake.

Samweli, alisema alipatiwa kifaa hicho ili kumsaidia kuandika kutokana na ulemavu wake wa mikono, unaomsababishia kushindwa kuandika.

Aidha, alisema baada ya kupewa, alikitumia kwa siku tatu na Mkuu wa Shule hiyo (hakumtaja jina), alianza kumpiga danadana akimwambia kifaa hicho ni mali ya shule na kipo kwa fundi, kwa ajili ya matengenezo.

"Baada ya kupigwa danadana nikaamua kunyamaza lakini napata wakati mgumu sana kwenye kuandika sababu siwezi lakini ipad niliweza kuandika kidogo," alisema.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Apael Akyoo, alisema mwanawe alisaidiwa na mzungu mmoja kupelekwa shule ya watu wenye ulemavu.

"Lakini baadaye nikasikia mzungu wake aliyempeleka shule amempa kifaa cha kumsaidia kuandika, lakini cha ajabu mwanangu alikitumia siku tatu nikaambiwa na mtoto kuwa amenyang'anywa na mwalimu hajapewa," alisema.

Alisema baada ya kusikia hivyo alisikitika na kuchukua hatua ya kumuuliza mmoja wa walimu ambaye alisema hawezi zungumzia chochote, kwa kuwa mwalimu mkuu wao aliamrisha kifaa hicho kikae shuleni na atakapokuja kila asubuhi apewe afanyie kazi.


"Nilipopewa jibu hili niliamua kunyamaza maana sikuwa na jinsi ya kufanya na mwanangu ameendelea kulalamika kuwa hapewi kifaa chake na anashindwa kuandika," alisema.

Mfadhili wa kifaa hicho (ipad), Gilbert Masawe, alisema mwaka jana 2022, alimpa ipad mwanafunzi huyo ili ikimsaidie kusoma na kuandika baada ya kugundua hawezi andika kwa njia ya kawaida.

"Lakini kwa sababu ya utunzaji mzuri tulishauri kifaa hiki kibaki shule atunziwe na anapofika asubuhi alewe aendelee na masomo na anaporudi nyumbani kibaki shule ila ni mali yake,"alisema.

Kwa mujibu wa Gilbert, hata yeye alisikia juu ya kutotumia mlengwa kifaa hicho na alimfuata mmoja wa walimu kuuliza juu ya hilo, lakini bado mwanafunzi huyo alisikia hakupatiwa kifaa chake.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo, Mkuu wa Shule hiyo, Jackline Mwanga, alikana tuhuma hizo, huku akisisitiza hakikutumika kwa mwezi mmoja kutokana na kufanyika kwa mitihani ya wilaya na mkoa, licha ya tuhuma hizo kudaiwa kuwapo kutoka mwaka jana.





# Wakumbushwa kutunza chakula kuepuka njaa

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamekumbushwa kutunza chakula kilichopatikana katika msimu huu ili kuepukana na tishio la njaa ambalo limekuwa likiibuka kila wakati baada ya kuuza mazao yao.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu hatua walizojiwekea kukabiliana na baa la njaa katika halmashauri hiyo, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Ushetu, Elibariki Leonard alisema wanaendelea na utoaji wa elimu kwa wakulima wao kwa kushirikiana na maofisa ugani wa kata lengo likiwa ni kuwahimiza kuuza na kutumia kiasi.

Alisema kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa katika msimu huu mavuno yapo kwa wastani kulinganisha na vipindi vya msimu uliopita.

Alisema ni vema wananchi wakafanya tathmini ya mahitaji ya familia zao kabla ya kuanza kuuza mazao waliyopata na hii itawasaidia kukabiliana na janga la njaa.

"Nyakati za mavuno wakulima wetu hujihusisha katika uuzaji wa mavuno wanayoyapata hali inayosababisha familia kukosa chakula kulingana na mahitaji ya kaya, hili limejitokeza msimu uliopita mpaka serikali kuuza mazao kwa bei ya chini, hili hatuhitaji lijitokeze, ndiyo sababu tunawakumbusha wakulima wetu kutunza chakula," alisema Leonard.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo aliiambia Nipashe kuwa kwa sasa katika vikao vya maendeleo ya kata ajenda ya utunzaji wa chakula ni ya kudumu.

Alisema msimu uliopita wananchi walihadaika na bei na kulazimika kuuza chakula walichokuwa nacho ndani na kusababisha serikali kuuza mahindi kwa bei nafuu kulinganisha na bei iliyokuwa sokoni.

Alisema hali hiyo ilisababisha Mbunge Cherehani kuwasaidia na kupata tani 100 za mahindi ili kuhakikisha wananchi wanakabiliana na njaa.

Mmoja wa wananchi hao, Jackson Wilison alisema: "Msimu uliopita nilipata mavuno mazuri lakini nilihadaika na bei iliyokuwapo na kuuza takribani mahindi yote, nikabakiza chakula kidogo, baada ya chakula hicho kuisha tuliangaika sana kwani hata bei za dukani zilipanda mara dufu."




Ofisa Rasilimali Watu wa Barrick North Mara, Daniel Paul, akizungumza na wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali vya mkoani Mwanza wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo lililoandaliwa na taasisi ya kimataifa ya vijana isiyo ya kiserikali inayohamasisha masuala ya uongozi na kujitolea kwa jamii ya AIESEC Tanzania na kudhaminiwa na kampuni ya uchimbaji madini ya Barrick, lililofanyika jijini Mwanza katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Aahidi kuipa nguvu kampeni ya msaada wa kisheria

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, ameiahidi Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na wadau wanaoshirikiana nao katika kuendesha 'kampeni ya kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia' kutoa ushirikiano ili kufanikisha kampeni hiyo kwa watu waishio pembezoni.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa utekelezaji wa kampeni hiyo kimkoa uliofanyika katika viwanja vya Sabasaba Shinyanga Mjini na kuzisisitiza kata zote kuhakikisha zinatenga maeneo maalum zitakapotolewa huduma hizo.

Alieleza kuwa kampeni hiyo inawakumbusha Watanzania wote uwajibikaji na usimamizi wa maamuzi yenye kuleta haki na akatumia fursa hiyo kuwambusha watumishi wote kutojihusisha na masuala ya rushwa inayosababisha kuzorotesha upatikanaji haki.

Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Pauline Gekul, alisema wizara itaendelea kushirikiana na mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhakikisha kampeni hiyo inatekelezwa ipasavyo ili kuwafikia Watanzania kwenye kata na mitaa yote nchini.

"Huduma ya msaada wa kisheria kuwafikia wananchi bure ni mapenzi na upendo wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa mwananchi wa hali ya chini hivyo lazima tuhakikishe tunatekeleza hitaji lake," alisema Gekul.

Meneja Rasilimali na Mawasiliano kutoka Shirika la Legal Services Facility (LSF), Jane Matinde, alisema kuwa uzinduzi wa kampeni ya msaada wa kisheria ya Rais Samia unakwenda kufanyika kila mkoa huku ikienda sambamba na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria ili kuchochea upatikanaji wa haki kwa wananchi hasa wasiojiweza ikiwamo wanawake, watoto na makundi maalum.

Alisema: "Tunafurahi kuona pia tumekuwa ni sehemu ya wadau muhimu katika utekelezaji wa kampeni hii nchi nzima tunaahidi kuendelea kuwezesha wasaidizi wa kisheria kwenye kila ngazi ya wilaya ili kusaidia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria bure kwa wananchi wote nchini."

# RC atangaza mwarobaini biashara magendo ya kahawa

**Na Titus Mwombeki,**
KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa ametangaza mbinu mbadala ya kudhibiti biashara ya magendo katika kahawa kuwa ni pamoja na vyama vya ushirika mkoani humo kufanya ushindani wa kibiashara kulinganisha na mataifa jirani.

Amesema hali hiyo itakayowasaidia wakulima wa zao hilo kuweka kipaumbele kwao na kuacha kusafirisha zao hilo nje kimagendo.

Aliyasema hayo juzi wakati akiongea na wanachama wa Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika mkoani humo.

Alisema kuwa suala la magendo limekuwa likiikosesha serikali mapato, chanzo kikiwa ni ukosefu wa ubunifu katika suala la bei ya kahawa nchini na kusababisha wakulima kuisafirisha nje kinyume cha sheria.

"Biashara ni ushindani hapa tuko mpakani tunaopakana nao ni wanunuzi na ni wauzaji wa kahawa wakubwa, niwaombe wafanyabiashara kuhakikisha mnanunua kahawa kwa bei sawa au kuzidi ya wafanyabiashara wa nchi za upande wa pili ili mkulima aone siyo tija tena," alieleza.

Alitaja njia nyingine kuwa ni pamoja na vyama hivyo kujitahidi kufanya maboresho katika suala la malipo kwa mkulima hususani pale anapowapelekea kahawa yake apatiwe pesa yake ndani ya saa 24.

Aidha, alisema kuwa serikali imeendelea kuwajali na kuwathamini wakulima wa kahawa kwa kuwaondolea vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na tozo ili wakulima hao waweze kunufaika na zao hilo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Kagera, Respicius John, alisema kuwa ushirika umefanikiwa kuwapatia mitaji midogo na ya kati wanaushirika na masharti nafuu ili kuweza kufanya kazi zao vizuri.

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kagera, Robert George, alisema kuwa ofisi yake inaenda kuwajengea uwezo wana ushirika katika utekelezaji wa majukumu yao huku akisema kuwa katika mkoa huo kuna vyama vya ushirika 369 vyenye wanachama 81,351, huku vyama 288 vikiwa hai na 81 vimekufa.



Ukurasa 14

Shinyanga kumekucha kutoka nyungu hadi chanjo UVIKO-19



Ukurasa 13

Siku ya Mazingira Duniani itumiwe kuyamulika haya...

Nipashe
TESA
Jumanne Juni 13, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Ukimya unapotawala mtaani, watu wasijisahau Uviko upo

ELIMU
NA ROMANA MALLYA

TUMBAKU NI MCHAWI

# Inawamaliza vijana, kukwamisha masomo, adui mkubwa mazingira

• Ni mkesha kuikausha, wazazi, watoto hakuna kulala

UNAPOZUNGUMZIA mapambano dhidi ya matumizi ya tumbaku huwezi kuacha kumtaja, Lutgard Kagaruki, ambaye takriban miaka 19 mfululizo ametumia muda wake kwa asilimia 100 kupiga vita kuvuta tumbaku.

Tafiti zinaonyesha ni moja ya chanzo cha magonjwa yasiyoambukiza ambayo kwa sasa yanaongoza kuua kuanzia saratani, shinikizo la damu, figo na changamoto za uzazi.

Lutgard ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF), alianza kampeni akiwa na miaka 53 na leo ametimiza miaka 72, akipigana vita, anasema kutumia tumbaku kumezidi na hali ni mbaya leo hususani vijana.

Mama huyu ni msomi akijihitimu diploma na shahada ya uzamivu nchini Uingereza ni mtaalamu wa tiba, akisomea Medical and Veterinary Parasitology, akijikita kwenye magonjwa ya binadamu na wanyama.

Lutgard amefanya kazi miaka 35 kwenye Maabara Kuu ya Mifugo ya serikali zamani Taasisi ya Utafiti wa Maradhi ya Mifugo, hadi kustaafu 2011.

Anakumbusha kauli mbiu ya mwaka huu ya siku ya kupinga matumizi ya tumbaku duniani: "Tunahitaji chakula na si tumbaku" na ya Afrika, "Licha Afrika siyo kampuni ya tumbaku."

"Sitaacha kupambano nilishaapa, ninawaambia watu kwa utani kwamba, nilishakubaliana na Mungu mpaka sheria itoke ikishatoka ndipo anichukue siwezi kuacha hili," Lutgard anasema.

Akizungumza na Nipashe kuelekea maadhimisho ya Kupinga Matumizi ya Tumbaku Duniani Mei 31, anakumbusha kuwa alianza vita mwaka 2004 kwa kupata mafunzo.

Anasema juhudi zilizofanyika tangu wakati huo ndizo zilizochangia mwaka 2010, kupata tuzo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuheshimu alichofanya.

### MAMBO YALIVYOKUWA

Wakati wanaanza hali ilikuwa tofauti katika matumizi ya tumbaku ikilinganishwa na sasa, leo hali ni mbaya kuitumia kumeongezeka, ikilinganishwa na awali.

"Kule Namtumbo ambako walikuwa wanalima tumbaku tulikoanza nao hadi kufikia 2015 zaidi ya asilimia 90 waliacha na kuingia kwenye kilimo cha mazao mbadala, mpaka sasa wananitafuta. Tulikuta wana nyumba za nyasi wakaezeka kwa bati, tena watoto hawakwenda shule wakaanza kusoma, wazazi walikuwa wanahonga walimu wasiende shule wakati wa kuvuna kwa sababu jani likikaa siku moja linaharibika." Anasema.



Lutgard Kagaruki. **PICHA: MTANDAO**



"Ukaushaji hutumia saa 24 familia nzima inawajibika kukesha kuchochea kuni mpaka ikauke, baba anachochea, baadaye mama na watoto wenye umri wa kwenda shule nao walikuwa na zamu tukawapa elimu mambo yakabadilika," anasema.

"Mkoani Tabora 2009 tulifanya utafiti asilimia 75 walitaka kuacha tumbaku muda mrefu, baada ya kuwapa elimu wako walioacha. Kuanzia 2015 hali imebadilika kulima tumbaku kumekuwa na hamasa kila kona," anaeleza.

Anasema mkutano wa tumbaku uliofanyika 2008 Afrika Kusini uliohudhuriwa na nchi zaidi ya 100 uliwekwa azimio kuwa ikifika 2030, dunia isiwe na tumbaku, lakini ilivyo anaona tatizo bado ni kubwa.

"Ninasema nyuma tulikotoka tulikuwa bora. Kwa sasa tunahamasisha watu watoke kwenye matumizi mbadala ya kuni na kuingia kwenye nishati safi ya gesi lakini Tabora na sehemu nyingine huwezi kuzuia kuni kama kilimo cha tumbaku hujakomeshwa.

"Lazima ikaushwe kwa moshi wa kuni, ndiyo wanaiita tumbaku bora na yenye bei. Lazima serikali ipige vita kilimo cha tumbaku ambacho ni chanzo cha uharibifu wa mazingira wakati ikihamasisha nishati mbadala. Madhara kiafya yanajulikana, mazingira yanaharibika, uchumi wa wakulima ni mdogo," anasema.

### KILIO MUSWADA

Lutgard anasema serikali inatakiwa kuhakikisha ule muswada ambao ulikamilika tangu mwaka 2017, unapelekwa bungeni kunusuru vijana walio waathirika wa matumizi ya tumbaku.

"Ukienda klabu kwenye maduka makubwa utanielewa,

INAENDELEA UK.12

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Ukimya unapotawala mtaani, watu wasijisahau Uviko upo

KWA Tanzania wengi wanaweza kudhani kuwa maradhi ya UVIKO-19 yametoweka, kwa taarifa si vyema kuchukulia poa. Corona ipo hivyo ni vyema kujihadhari kama kukumbuka kunawa muda wote na kuvaa barakoa hasa hospitalini.

Itakumbukwa kuwa Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema zaidi ya maambukizi mapya milioni 1.7 na vifo zaidi ya 10,000 vinavyotokana na UVIKO-19, vimeripotiwa katika siku 28 zilizopita kuanzia Mei 8 hadi Juni 2023.

Aidha, linatangaza kuwa vimepungua kwa asilimia 38 na 47 ikilinganishwa na siku 28 zilizopita kuanzia Aprili 10 hadi Mei 7, 2023 na kwamba, katika kipindi hiki cha siku 28 cha kuripoti, maeneo 144 kati ya 243 yaliripoti angalau kesi moja.

Shirika la Afya linasema kuwa hali katika kanda zake inaonyesha kupungua kwa kesi na vifo katika kanda zote sita za WHO na kwamba kufikia Juni 4, 2023, zaidi ya wagonjwa milioni 767 walithibitishwa na zaidi ya vifo milioni 6.9 vimelitokea na kuripotiwa duniani kote.

Virusi vyote pamoja na SARS-COV-2, vinavyosababisha COVID-19, hubadilika kadri muda unavyopita. Mabadiliko mengi hayana athari kubwa kwa hali ya virusi.

Hata hivyo, baadhi ya mabadiliko yanaweza kuathiri mwenendo wa virusi, kama vile jinsi vinavyoenea kwa kasi, urahisi, ukali wa ugonjwa unapoingia mwilini, utendaji kazi wa chanjo, dawa za matibabu, mbinu za uchunguzi na hali ya afya ya umma na jamii. Ni taarifa ya WHO inayoitwa "Weekly epidemiological update on COVID-19 - 8 Juni 2023"



Mgonjwa wa UVIKO-19 akiwekewa mashine ya kupumulia. **PICHA: MTANDAO**

### KIRUSI KINACHOTESA

Historia inaonyesha kuwa Novemba 2022 Shirika la Afya Duniani linakitaja kirusi cha omicron kuwa ni kirusi hatari zaidi na kinachoibua wasiwasi mpya duniani kuhusu kitisho cha COVID-19.

Aina hiyo ilitambuliwa kwa mara ya kwanza Afrika Kusini na Botswana ikaripotiwa takribani mataifa 190 baadaye na nchini Marekani ndani ya majimbo yote 50 na huko Washington, D.C jiji maarufu duniani.

Omicron inaelezwa kuwa ina uwezo wa kubadilika takriban mabadiliko 50 na kujiunda upya na kuwa kirusi hatari zaidi mwishoni mwa mwaka jana. Katika kubadilika huko hakukuonekana kwa pamoja hapo awali, ikiwa ni pamoja na mabadiliko 30 katika jeni ya protini ambayo virusi vya corona hutumia kushikamana na seli za binadamu.

Protini za omicron zina mabadiliko kadhaa ambayo yanadhaniwa kufanya virusi kuambukiza zaidi, ikiwa ni pamoja na aina za D614G, N501Y na K417N, yote hayo ni majina ya kitaalamu na kimaabara zaidi.

Kabla ya omicron kilikuwa kirusi delta kikianza kutawala Marekani wakati wa kiangazi cha mwaka 2021, lakini Omicron sasa ameipita makali kulingana na makadirio ya Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa.

Mnamo Machi 15, 2023, WHO inatangaza kwamba herufi za Kigiriki zitapewa majina kwenye virusi jamii ya VOCs, wakati VOI jina litarejelewa kwa kutumia mifumo ya majina ya kisayansi yaliyoyaanzisha uchunguzi kama vile majina ya 'Nextstrain na Pango' mfano XBB.1.5/23A kwa jamii ya VOI iliyogunduliwa karibuni.

Taarifa kutoka Marekani zinazotolewa na mtandao wa tiba wa Jimbo la Nebraska, unasema kwa sasa, kirusi kikuu nchini Marekani ni XBB.1.5, kinachoelezwa kuwa kina na wagonjwa walioripotiwa ni asilimia 53.8, kikifuatiwa na aina ya XBB.1.16, yenye asilimia ya wagonjwa 15.1 na kingine ni XBB.1.9.1 chenye asilimia 11.8 ya kesi au wagonjwa.

"Kirusi asilia omicron kimetoweka sasa," anasema Dk. Rupp. "Kwa sasa vitoto vyake ndivyo vinavyozunguka, ikiwa ni pamoja na XBB.1.5, XBB.1.16 na XBB.1.9.1."

### KUTAMBUA TOFAUTI

Ni swali linaloulizwa na wengi unaweza kutambua una kirusi kipi? Ukweli ni hapana unapofanyiwa kipimo cha COVID-19, hutagundua ni kirusi gani kilichokusababishia maambukizi. Hiyo ni kwa sababu vipimo vya COVID-19 hutambua uwepo wa virusi pekee havibainishi jamii au vitoto vinavyoletwa na kizazi kipya, inasema WHO.

Kwa hali hiyo watu waendelee kukumbuka kuwa COVID-19 ni pasua kichwa na kwamba kujikinga ni lazima.

## Inawamaliza vijana, kukwamisha masomo, adui mkubwa mazingira

INATOKA UK.11

vijana wanavuta shisha na zimewekea ladha tofauti zinazoleta hamasa kwao kutumia. Ni lazima taifa lione namna ya kuwanusuru."

### KUANZA KAMPENI

"Miaka miwili kabla ya kustaafu nilianza kuvutiwa na mambo ya tumbaku baada ya kujifunza vitu vingi vinavyoihusu. Nikaomba likizo bila malipo nikajikita zaidi kwenye eneo hili.

"Na baada ya likizo niliporudi kazini nikawa sina hamu tena na mambo ya maabara akili ikawa imehamia kwenye tumbaku na hapo nilikuwa nimeshawatembelea wakulima wa Namtumbo nikakuta wanateseka nikaongea nao wakaanza kubadilika," anasimulia.

Anaongeza: "Bado ninakumbuka nilikotoka nilikuwa ninatembea sana kwa Wamasai, mifugo yote nilikuwa ninaijua, ulikuwa ukiniuliza kupe wote waliopo Tanzania niliwajua. Tulikuwa tunaangusha ng'ombe tunachukua damu na kupe tunakuja kuangalia magonjwa."

### MBOBEZI MAPAFU

Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mfumo wa Mapafu, Mwanaada Kilima, kutoka Idara ya Magonjwa ya Ndani Kitengo cha Mapafu, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), anasema magonjwa yanayotokana na matumizi ya tumbaku yanaongezeka.

"Tunachokiona ni idadi kubwa ya magonjwa ya mapafu, maradhi ya moyo, shinikizo la damu na saratani yanaongezeka. Kwa wastani wanaoathirika zaidi ni vijana wenye umri unaoanzia miaka 35 kuendelea.

"Kwa sasa magonjwa yasiyoambukiza yanawaathiri walioko chini ya miaka 60. Rika linalotumia zaidi tumbaku ni vijana na kwa bahati mbaya kuna aina nyingine ya matumizi ya tumbaku inayoitwa shisha," anasema Mwanaada.

Mbobezi huyu ni Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani (APHYTA), anasema kumekuwa na mlipuko wa matumizi ya tumbaku kupitia shisha ambao kiasi kikubwa inawatia wasiwasi hali ya afya ya vijana na wazee miaka ijayo.

"Sisi madaktari tunaona wagonjwa kila siku na athari kubwa wanazozipata, wito wetu ni kwamba matumizi ya tumbaku yapigwe marufuku. Mfano kijana akikaa akavuta bomba la shisha akimaliza mtungi ni sawa na kuvuta zaidi ya sigara 20.

"Athari ni kubwa kuliko akivuta sigara za kawaida, ambazo zinatumika kwa kasi na uvutaji kwa sasa vijana wanahamasishana. Hii inatia wasiwasi," anasema mtaalamu huyu.

Anatoa mfano wa kijana wa miaka 38 aliyefika hospitalini hapo akiwa ameathirika na pafu la kushoto lilikuwa halifanyi kazi bila msaada wa oksijeni.

"Ilibidi kuliondoa ili kuliokoa la upande wa kulia na operesheni yake ni gharama si chini ya Sh. milioni 10. Mpaka sasa yupo katika tiba kwa sababu baada ya kufanyiwa upasuaji anaendelea na matibabu kuhakikisha anatengemaa."

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Siku ya Mazingira Duniani itumiwe kuyamulika haya...

TAIFA linapoadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, Juni 5, Watanzania wanasimama kifua mbele kwa vile zipo maliasili za kutosha kuanzia watu zaidi ya milioni 60, ardhi ya kawaida na oevu, maji, wanyama wa kufugwa na wa porini, samaki na viumbe wengine waishio majini yakiwa ya chumvi na ya baridi, miti, misitu na madini aina mbalimbali.

Kati ya maliasili hizo, zipo zinazomilikiwa na serikali na kusimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa niaba ya Watanzania wote na hizo ni pamoja na misitu, wanyamapori, malikale pamoja na zile zinazohusiana na shughuli za utalii.

Tangu Uhuru takribani miaka 62 iliyopita, juhudi zimekuwa zikifanyika kuhakikisha maeneo yaliyohifadhiwa kisheria yanatunzwa na kusimamiwa ipasavyo kwa kuzuia shughuli za kibinadamu.

Hata hivyo, kumekuwapo na changamoto lukuki katika harakati za kutimiza nia hiyo njema kwa mustakabali wa taifa letu, baadhi ya changamoto ni pamoja na wataalamu wa kusimamia misitu ya asili kuwa wachache.

Aidha, kutengewa fedha kidogo kutunza na kuilinda misitu husika hivyo kushindwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kwa ufupi, misitu ya asili iliyohifadhiwa kisheria, imekuwa kama "shamba la bibi" kwa maelezo kwamba haina ulinzi wa uhakika, mipaka yake imetelekezwa kwa muda mrefu kiasi cha watu kushindwa kuitofautisha na maeneo huria.

Serikali ilipoidhinisha sera iliyopelekea baadhi ya taasisi na idara zake zilizokuwa na mlengo wa kibiashara na kuzitaka kuendesha shughuli zake kibiashara kupitia "wakala" au "mamlaka"; hivyo ndivyo Idara ya Misitu na Nyuki ilivyotafsiriwa na kuonekana inafaa kuwa 'Wakala wa Serikali' badala ya kuendelea kuwa idara.

Mwaka 2010 'Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania' (TFS) ikaanzishwa rasmi. Hata hivyo, nikiri kwamba baadhi ya wadau na viongozi serikalini walitoa angalizo kwamba 'kuweka misitu ya asili chini ya wakala ni kuiweka katika hali ya kuharibika zaidi'.

Kwa kuzingatia uhalisia wa masuala ya



Mkaa kila mahali kwenye pikipiki, baiskeli na malori ni mamilioni ya miti yanayokatwa kwenye misitu ya asili. **PICHA: MTANDAO**

Wakala au Mamlaka ilidhaniwa misitu ya asili itakuwa katika mikono salama, kwa mantiki kwamba uwezo wa kuisimamia na kuitunza utaongezeka kuliko ilivyokuwa chini ya idara.

Sasa ni takribani miaka 13 tangu kuanzisha wakala na uzoefu unaonyesha kuwa hali ya misitu ya asili imeporomoka zaidi isipokuwa maeneo machache, kama asilia mia tano pekee ya misitu iliyohifadhiwa nchini.

Misitu hiyo ilibadilishwa hadhi yake kuwa Misitu ya Hifadhi-Asilia (Nature Forest Reserves) ambayo hali yake ni afadhali kidogo ukilinganisha na iliyobaki.

Ukitafakari kwa undani utaona Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, kwa kiasi kikubwa umejitahidi kuboresha mashamba ya miti (forest plantations) lakini kwa upande wa misitu ya asili hali siyo nzuri.

Kasi ya kukata miti ya asili imeongezeka kiasi cha kutishia taifa kugeuka jangwa. Hali hiyo imesababisha baadhi ya maeneo kubadilishwa kuwa sehemu ya 'Mapori ya Akiba' chini ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), lakini kwa nia njema ya kuyanusuru yasiendelee kuharibiwa kupitia shughuli za kibinadamu kama kukata miti, kutengeneza mkaa, kuvuna magogo na nguzo kiholela pamoja na kilimo na ufugaji usiodhibitiwa.

Iwapo dhamana ya wakala ilikuwa kuongeza nguvu katika kuisimamia misitu ya asili ili taifa liendelee kunufaika na huduma za misitu za kiikolojia na uhifadhi wa viumbe adimu duniani, ikiwamo viumbe vinavyopatikana hapa nchini tu (siyo mahali pengine duniani) pamoja na kutunza mazingira kwa kuimarisha mchango wa miti au misitu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Wakala wamekwama wapi? Pengine hii inaashiria kuwa waliokuwa na 'hofu' kuhusu kuifanya Idara ya Misitu na Nyuki' kuwa wakala walikuwa wameona mbali.

Wataalamu wa misitu katika wakala wamekuwa 'jeshiusu' au nusu jeshi lakini kwa wataalamu wa misitu walioko kwenye halmashauri za wilaya, zenye maeneo makubwa ya misitu ya asili, ambao pia ni wachache mno hawamo kwenye mfumo wa 'jeshiusu' isitoshe hawawezeshwi inavyostahili.

> Wakala wamekwama wapi? Pengine hii inaashiria kuwa waliokuwa na 'hofu' kuhusu kuifanya Idara ya Misitu na Nyuki' kuwa wakala walikuwa wameona mbali.

Mathalani, bajeti yao ni ndogo na kwa uzoefu uliopo hata kupata kilichotengwa ni shida mno pamoja na hayo, sekta ya misitu na nyuki siyo mojawapo ya vipaumbele muhimu vya taifa kama ilivyo kwa sekta za elimu, afya, maji, nishati, miundombinu na kilimo.

Hali hiyo inatokana na mitazamo ya kisera, siasa, kijamii na kama Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alivyowahi kusema "kupanga ni kuchagua" hivyo, matumizi ya rasilimali fedha na nyenzo muhimu vinaegemea katika mitazamo hiyo.

Hivyo, inavyoelekea kutunza na kuisimamia misitu ni kwa kudra za Mwenyezi Mungu tu, kimsingi, wataalamu wa misitu kuwa 'jeshiusu' ni suala la msingi kuwafanya wawe wakakamavu na kuweza kuitunza misitu ipasavyo. Lakini hilo pekee haliwezi kuimarisha ulinzi wa misitu iwapo inabaki imetelekezwa kutokana na wataalamu kuishi mbali na maeneo yaliyohifadhiwa.

Kuanzisha wakala kulilenga wataalamu tufanye kazi tukiwa katika maeneo yanayohusika, lakini wakala ulianza na mtazamo tofauti 'kukusanya mapato na kuishi mbali na maeneo yaliyohifadhiwa.

Kukusanya mapato ni jambo jema ila inatakiwa hilo liwe ni mojawapo ya juhudi za kitaaluma kuitunza, kuisimamia na kuhakikisha misitu inatumika kwa njia endelevu.

Kinyume cha hapo ndiyo hali tunayoishuhudia sasa kwenye misitu ya asili, mwenye nguvu anafanya anavyotaka bila kizuizi. Wakala pia kuweka juhudi kwenye mashamba ya miti ni suala la kupongeza.

Hata hivyo, kama taifa tunahitaji kubadilika kimtazamo na kisera kiasi kwamba kupitia Sera ya Taifa ya Kushirikisha Sekta Binafsi (public-private partnership), mashamba ya miti yakiwekwa kwenye usimamizi na uendelezaji wa sekta binafsi, wakala akibaki na jukumu la kusimamia na kukusanya mapato, siyo siri taifa litanufaika zaidi kuliko ilivyo sasa. Kupanua mashamba na kuuza miti kwa sekta binafsi ilikuwa ndilo jukumu la idara, tulitegemea wakala wafanye zaidi ya hapo na kuuza bidhaa za misitu zilizoongezwa thamani. Vilevile, kuendelea kukinzana na sekta binafsi wakala ikiwa mshindani wao (competitor) hapo kuna walakini ni vyema tukarekebisha.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Shinyanga kumekucha kutoka nyungu hadi chanjo UVIKO-19

UVIKO -19 ulioanza Desemba 2019, ukisambaa dunia nzima unasadikiwa kuua takriban watu 180,000 kwa mujibu wa Shirika la Afya Dunia (WHO), ambao pia liliutangaaza kuwa janga la dunia.

Machi 15, mwaka 2020, aliripotiwa mgonjwa wa UVIKO-19 jijini Arusha, ambaye alitokea nchini Ubelgiji na Shirika la Ndege la Rwanda.

Baada ya kuwapo UVIKO taifa halikaa kimya utoaji chanjo ukaanza japo kukiwa na upotoshaji kwa wananchi kuwa wakichanjwa watakuwa mazombi, kupungukiwa na nguvu za kiume, kujifungua watoto wenye ulemavu, pamoja na kupunguza maisha.

Hofu ya upotoshaji huo ikaathiri kasi ya utoaji chanjo wananchi, hasa wazee na vijana wakiogopa kumalizika nguvu za kiume na kupunguza maisha. Imani ambayo inakanushwa na wataalamu pamoja na wale ambao wameshapata chanjo.

Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma mkoani Shinyanga, Mwita Thomas, anasema utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 umefikia kwa asilimia 100 na kwa mwaka 2023 wamejiwekea malengo ya kufikia asilimia 120 na hadi Februari wamefikisha asilimia 108.

"Utoaji chanjo ya UVIKO-19 unakwenda vizuri, lakini kwa wazee na vijana wanasuasua kuchanja, naombeni wanahabari tumieni taaluma yenu kuondoa upotoshaji ili watu wapate huduma na inatolewa bure kwenye vituo vyote vya afya," anasema Mwita.

Katibu wa Baraza la Wazee Mkoa wa Shinyanga, Anderson Lyimo, anasema imani potofu imekuwa kikwazo kikubwa kwa wazee kuchanjwa licha ya wengi wao kujitokeza, lakini wale wa vijijini wamekuwa wagumu.

Anasema serikali na wadau wa masuala ya afya wanapaswa kutoa elimu zaidi kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19 kwa wazee na vijana hasa wa maeneo ya vijijini, ambao tayari wameshaathiriwa na imani potofu dhidi ya chanjo.

Lyimo ambaye ni Katibu wa Baraza la Wazee Taifa, anashangaa baadhi ya wazee kuogopa kupata chanjo ya UVIKO-19 na wakati mwili mwao tangu walipozaliwa wamechanjwa chanjo nyingi na kama kungekuwa na nia ya kuwaua wangekuwa na nia ya kuwaua si wangewaua siku nyingi na kuwataka wapuuze upotoshaji bali wajitokeze kuchanjwa.



Lucia Luziga mkazi wa Didia wilayani Shinyanga (kulia), akichanjwa baada ya kuhamasishwa na kuondolewa imani potofu. Kushoto ni Ofisa Afya Kata ya Didia, Edwardina Maganga. **PICHA: MARCO MADUHU**

> "Utoaji chanjo ya UVIKO-19 unakwenda vizuri, lakini kwa wazee na vijana wanasuasua kuchanja, naombeni wanahabari tumieni taaluma yenu kuondoa upotoshaji ili watu wapate huduma na inatolewa bure kwenye vituo vyote vya afya.

"Nimechanjwa UVIKO-19 tangu Agosti mwaka 2021na sijapata madhara hadi sasa na afya yangu ni imara na baadhi ya magonjwa madogo ambayo yalikuwa yakinisumbua awali mfano mafua na vikohozi sijayaona, hivyo nawasihi wazee wenzangu hasa wa vijijini jitokezeni mpate chanjo ni salama na haina madhara yoyote puuzeni imani potofu,"anasema Lyimo.

Wilaya ya Shinyanga ni miongoni mwa maeneo ambayo wananchi wake wa vijijini hasa wazee, vijana na wanawake wameathiriwa na upotoshaji wa chanjo ya UVIKO-19 na kusababisha kusua kupata chanjo hiyo kwa hofu iliyojengeka kuwa watapata madhara.

Katibu wa Baraza la Wazee Kata ya Didia wilayani Shinyanga, Engelbert Kidutu, anasema awali hakuwa tayari kuchanja chanjo ya UVIKO-19 kutokana na kuenea kwa imani potofu kuwa mzee akichanja viungo vyake vinadhoofika, atapunguza siku za kuishi na kupungukiwa nguvu za mwili.

Anasema baada ya kupata elimu kwamba hakuna madhara kwa wazee, bali ni kinga dhidi yao kutokana na kinga zao kushuka na siku wakipata maambukizi ya virusi vya corona wanakuwa katika hatari kubwa ya kupoteza maisha ndipo akaamua kuchanja.

"Kusema ukweli mimi sikuwa tayari kupata chanjo kutokana na maneno ya mitaani ambayo yanaenezwa kuwa chanjo zina madhara na hata mke wangu alivyochanjwa na kumuona afya yake nzuri nilikuwa bado siamini, lakini sasa nimepata elimu na nimeamua kwa hiari yangu," anasema Kidutu.

### HOFU KINAMAMA/VIJANA

Lucia Luziga mkazi wa Didia wilayani Shinyanga, anasema hakuwa anafikiria kuchanja UVIKO-19, kutokana na uvumi kuwa mwanamke akichanja hawezi tena kujifungua watoto na kama akijifungua basi watakuwa walemavu.

Anasema baada ya kupata uhamasishaji kuwa hakuna madhara kutoka kwa wataalamu wa afya na ushuhuda kwa wanawake ambao wameshachanjwa na wamejifungua watoto wakiwa wazima wa afya njema, ndipo naye amegusiwa na kuamua kupata chanjo ili imlinde dhidi ya maambukizi ya UVIKO.

Kijana Joseph Machibya mkazi wa Tinde wilayani Shinyanga, anasema vijana wengi wa maeneo ya vijijini hawana imani na chanjo kwani wanakosa elimu sahihi ya na wamekuwa wanaogopa kuchanja wakihofia kupungukiwa na nguvu za kiume na kushindwa tendo la ndoa.

Ofisa Afya Kata ya Didia, Edwardina Maganga, ambaye amekuwa akitoa chanjo ya UVIKO-19 vyumba kwa vyumba wilayani humo, anasema imani potofu imewaathiri wananchi wengi hasa wazee na vijana na kushindwa kujitokeza kupata chanjo.

Anasema wakati wakitembea nyumba kwa nyumba kutoa chanjo na kabla ya kuanza kuchanja wamekuwa wakitoa elimu kwanza ili kuondoa upotoshaji, ndipo wananchi wanakubali kupata chanjo hiyo ambayo wanaitoa ni ya Jonson Jensen (JJ) ya dozi moja ili wasipate usumbufu kutafuta dozi ya pili.

"Elimu ikitolewa kikamilifu maeneo ya vijijini wananchi wapo tayari kuchanjwa, sisi tumetembea nyumba kwa nyumba kutoa elimu na tumechanja watu wengi wakiwamo wazee na vijana na hakuna ambaye amelalamika kupata madhara ya kiafya," anasema Edwardina.

"Mtu akipata chanjo yoyote ile mwilini lazima awe na maudhi madogo sababu kitu kigeni kimeingia mwilini lakini chanjo zote hazina madhara sababu zichunguzwa na kuthibitishwa kutumika, naomba wananchi waendelee kupata chanjo sisi tupo tayari kutoa huduma," anaongeza Edwardina.

Mtendaji wa Kata ya Didia Monica Mpolosi, anasema imani potofu juu ya chanjo ya UVIKO-19 zimeathiri sana wananchi wa maeneo ya vijijini, kwa kuelezwa kuwa chanjo ni Freemasoni, lakini kwa kushirikiana na viongozi wenzake na wataalamu wa afya, wamefanikiwa kupunguza imani hizo na bado wanaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa chanjo.

Shirika la Women Elderly Advocacy and Development Organization (WEADO) la mkoani Shinyanga, linaunga mkono juhudi za serikali kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19 mkoani Shinyanga, ili wananchi wajitokeze kupata chanjo hiyo sababu COVID-19 bado ipo, kwa mujibu wa takwimu ambazo zimetolewa hivi karibuni na Wizara ya Afya.

Ofisa Miradi wa WEADO, Winnie Hinaya, anasema kampeni hiyo wataitekeleza kwa muda wa miezi mitatu katika kata sita za wilayani Shinyanga, ambazo ni Tinde, Didia, Masengwa, Usanda, Iselamagazi na Solwa na baada ya hapo wataenea kwenye kata zote wilayani humo ili wananchi wapate chanjo na kuwa mabalozi wa uhamasishaji chanjo.

Anasema chanjo ya UVIKO-19 ni muhimu katika kukabiliana na ugonjwa wa corona, sababu watu ambao wamekuwa wakipata maambukizi na wamechanjwa hawezi kuwa katika hatari kubwa ya poteza maisha, tofauti na wale ambao hawajachanjwa ambao maisha yao yapo hatarini na ndiyo maana wamekuja na mradi wa kampeni ya hamasa ya chanjo kwa wananchi.



## Aomba serikali, viongozi dini kuangalia makundi maalumu

**Na Peter Mkwavila,**
MPWAPWA

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini Taifa Makanisa ya Revival Evangelistic Assemblies of God Tanzania (REAGT), Askofu Jackson Madelemo, ameiomba serikali na viongozi wa madhehebu ya dini nchini kuwaangalia na kuwapatia misaada makundi mbalimbali ya wasiojiweza wanaoishi vijijini ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Askofu Madelemo, alitoa rai hiyo juzi baada ya kuwapatia misaada ya vitu mbalimbali ikiwamo chakula kwa makundi mbalimbali yenye uhitaji wakiwamo wajane yatima na wasiojiweza waishio vijijini iliyotolewa na washirika wa kanisa hilo lililopo Mtera Staaf wilayani Mpwapwa.

Akizungumza kwenye ibada ambayo ilikuwa maalumu kwa ajili ya tamasha la uimbaji na ugawaji wa misaada hiyo, askofu huyo aliiomba serikali na viongozi wa madhehebu ya dini kuwaangalia na kuwasaidia makundi hayo ambayo kwa asilimia kubwa yamesahaulika huko vijijini, alisema wajibu wa kuwaangalia na kuwasaidia upo mikononi mwa viongozi wa ngazi mbalimbali pamoja na watu wenye vipato ikiwamo serikali badala ya kusubiri wafadhili kutoka nje ya nchi.

Alisema, makundi hayo yapo pia kwa mpango wa Mungu wanahitaji kupatiwa misaada mbalimbali ikiwamo ya kiafya, kielimu, chakula, matibabu ili waweze kuondokana na umaskini ambao umekuwa ukiwaandama walio wengi ndani ya familia zao.

"Niwaombe viongozi wa madhehebu ya dini waumini wenye kipato na serikali yenyewe tuwaangalie watu hao kwa jicho la pili hususani hawa wanaoishi vijijini bado walio wengi wanahitaji kusaidiwa misaada mbalimbali ikiwamo ya kiafya, chakula, mavazi na elimu," alisema.

Pia alisema kanisa lake limejiwekea utaratibu wa kila mwaka kukusanyika na makundi mbalimbali bila kujali itikadi yoyote kwa ajili ya kuwapatia misaada hiyo na kula chakula cha pamoja.

Aliwataka kuongeza nguvu zaidi ya kushirikiana na serikali katika shughuli za kimaendeleo ikiwa na pamoja kuiombea serikali na viongozi waliopewa dhamana ya kuiongoza nchi.

# DC Kongwa atoa siku 7 wananchi wapatiwe Vitambulisho vya Taifa

**Na Renatha Msungu,**
KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Remidius Mwema, ametoa siku saba kwa watendaji wa kata, vijiji na mtaa, wananchi wao wanapatiwa Vitambulisho vya Taifa.

Mwema, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa ugawaji vitambulisho hivyo kwa wakazi wa maeneo hayo katika Uwanja wa Aman, mji mdogo wa Kibaigwa wilayani hapo.

Alisema mpaka sasa ni watu 65,334 kati ya 120,702 walioijiandikisha na waliokamilisha taratibu za kupata vitambulisho hivyo wanapaswa kupatiwa.

"Naomba watendaji wa kata, vijiji na mtaa, mkasimamie suala hilo nahitaji kuona wananchi wamepatiwa vitambulisho vyao vya NIDA, ndani ya muda huo," alisema Mwema.

Alifafanua kuwa kazi hiyo itakuwa endelevu huku akiwasisitiza kusimamia kila vitambulisho hivyo vinapokuwa tayari wahakikishe wananchi wa maeneo hayo wanapata.

Pia aliwataka wananchi kuzingatia matumizi sahihi ya vitambulisho hivyo kwa sababu ni njia pekee ya kufanikisha lengo la kitaifa la kuboresha utoaji huduma kwa wananchi wake kupitia vitambulisho hivyo.

Awali, akiwasilisha taarifa ya NIDA, Ofisa Msajili Vitambulisho vya Taifa wa Wilaya ya Kongwa, Said Hamad, alisema jumla ya vitambulisho 120,702 vimezalishwa wilayani Kongwa huku 100,334 vimekamilika sawa na asilimia 83 tangu kuanza kwa mpango huo.

Alisema kazi hiyo inaendelea vizuri kwa upande wa eneo hilo huku akisisitiza watu wote walioomba vitambulisho hivyo kupatiwa kwa wakati sahihi vinapokuwa vimekamilika.

Kaimu Meneja wa Udhibiti na Usambazaji wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Makao Makuu, Balbina Mtui, aliwataka wananchi kutambua kuwa Kitambulisho cha Taifa ni nyara ya serikali kinatumiwa na mtu moja na mwiko kukitumia vinginevyo.

Alisema wananchi wenye namba za NIDA wanaosubiri vitambulisho wanaendelea kupatiwa huduma zote muhimu sawa na walio na vitambulisho, hawapaswi kuwa na wasiwasi.

Alifafanua kuwa mamlaka hutoa vitambulisho aina tatu kwa lengo la kuwatambulisha wananchi wazawa, wageni walioppo nchini na wakimbizi wanaoishi kisheria.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti ya Shirika la Posta, ofisa kutoka Shirika hilo, Stephen Kibona, aliwaambia wananchi kuwa NIDA imeingia ubia na Shirika la Posta katika usambazaji wa vitambulisho na kwa kupitia mfumo wa anwani za makazi, shirika litawafikishia hadi mahali walipo.

Alisema wananchi wanapaswa kujitokeza kwa ajili ya kujiandikisha ili wapate vitambulisho hivyo na namba za NIDA kwa sababu watafikishiwa popote walipo vitakavyokamilika.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Taifa Makanisa ya Revival Evangelistic Assemblies of God Tanzania (REAGT), Askofu Jackson Madelemo, akimkabidhi mmoja wa waumini wa kanisa hilo msaada kwenye ibada maalumu iliyokuwa kwa ajili ya tamasha la uimbaji na ugawaji wa vitu mbalimbali iliyofanyika katika Kanisa la Mtera Staaf wilayani Mpwapwa jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Manyoni yaja na 'wawili kwa wawili'

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

SHUJAA wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), Kata ya Manyoni mkoani Singida wameanzisha kampeni ya kuongeza mashujaa kwa kila nyumba kwa ajili ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia inayojulikana 'Wawili kwa Wawili'.

Makamu Mwenyekiti wa SMAUJATA wa kata hiyo, Wallece Shechambo, alisema hayo jana walipokuwa wanashiriki shughuli ya kijamii ya ujenzi wa madarasa katika shule mpya ya msingi ya Muungano Maghorofani katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Alisema kampeni hiyo ya 'two by two' imelenga kuongeza mashujaa wa mapambano ya kutokomeza vitendo vya ukatili katika kata hiyo na maeneo mengine yote ya Wilaya ya Manyoni.

"Kampeni hii tumeipa jina la wawili kwa wawili, 'Two by Two' yaani tutapita kila kaya iliyopo ndani ya kata yetu kutoa elimu ya kupinga ukatili na kuhamasisha watu wawili katika nyumba husika wawe mashujaa ambao nao watakwenda kwenye kaya iliyo jirani nao kutafuta mashujaa wawili hadi kila nyumba iwe na mashujaa hao," alisema.

Sechambo alisema kampeni hiyo itasaidia kuwa na mashujaa kila nyumba wa kupinga ukatili na kuwa kama kata yao itakuwa na kaya 10,000 basi na mashujaa watakuwa 20,000 jambo litakalosaidia kutokomeza kabisa vitendo hivyo kama sio kuvipunguza.

Alisema mashujaa watakaopatikana kwenye kaya hizo wanaweza kuwa baba na mama, wasichana au wavulana bila kujali elimu na taaluma zao ili mradi tu waweze kupaza sauti ya kufichua vitendo vyote vya ukatili na kutoa taarifa kwenye vyombo husika kama ofisi za kata na dawati la jinsia lililopo katika vituo vya polisi na kwa maofisa ustawi wa jamii.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Mwembeni, Saluthary Naaly, alisema moja ya kazi ya mashujaa wa SMAUJATA ni kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii ambapo wataweza kukutana na wananchi na kuwapa elimu hiyo ya kupinga ukatili.

Katibu wa SMAUJATA wa kata hiyo, Sarah Yohana, alisema changamoto kubwa iliyopo kwa baadhi ya wanamume ni kuwabana wake zao na kushindwa kushiriki katika mambo mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali na kupinga ukatili.

Makamu Katibu wa SMAUJATA wa kata hiyo, Joyce Peter, alisema kuna faida kubwa ya kushirikiana baina ya familia na familia katika shughuli mbalimbali ziwe za huzuni, furaha na maendeleo jambo kubwa likiwa ni kudumisha upendo.

Mjumbe wa SMAUJATA wa kata hiyo, Neema Masabuni, alizungumzia kuhusu madhara yanayoweza kutokea kutokana na kutokuwapo kwa ushirikiano katika jamii na kuwa siku zote utengano ni udhaifu.

Mjumbe wa SMAUJATA wa kata hiyo, Matilda Musa, alizungumzia kuhusu wajibu wa kuwa na uhusiano mzuri katika familia huku mjumbe mwenzake Zena Salimu akihimiza suala zima la kufichua vitendo vya ukatili.





# Naibu Waziri wa Maji atoa msaada Sh. milioni 7 UWT

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ametoa msaada wa Sh. milioni saba kwa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Mbeya Mjini, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba ya katibu wa umoja huo pamoja na kitega uchumi.

Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, alitoa msaada huo juzi aliposhiriki Baraza la UWT la Wilaya ya Mbeya Mjini ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake ya kutoa Sh. milioni 20 kwa kila wilaya katika mkoa huo.

Akizungumza wakati akikabidhi fedha hizo, Mahundi aliupongeza umoja huo kwa kuanzisha mradi huo wa nyumba za kupangisha ambao alisema ukikamilika utakuwa ni miongoni mwa vyanzo vya mapato vya uhakika.

Alisema kabla ya kwenda kwenye baraza hilo alitembelea mradi huo na kubaini kwamba mradi unaendelea vizuri na hivyo akaona ni vizuri kuwashika mkono ili kasi iongezeke.

Alisema baada ya kutoa fedha hizo UWT Mbeya Mjini watakuwa wanamdai Sh. milioni 13 ambazo aliahidi kuwa atazikamilisha hivi karibuni.

"Nawapongeza sana kwa mradi huu, sikuwa na lengo la kuwapa fedha zote hizi lakini baada ya kutembelea nimeridhika na nikawaambia wasaidizi wangu kwamba nachukua fedha kwenye fungu lingine ili zifike hizi nilizowapatia," alisema Mahundi.

Aliwataka wadau mbalimbali kuendelea kuusaidia umoja huo ili ukamilishe mradi huo mapema na uanze kufanya kazi ya uzalishaji na kuufanya kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato vitakavyoufanya kujitegemea. Hivyo, aliutaka umoja huo pia kuendelea kuwaombea viongozi mbalimbali wa serikali ili watekeleze majukumu yao vizuri na kulifanya taifa kuwa na amani na utulivu.

Katibu wa UWT Wilaya ya Mbeya Mjini, Ruth Mwambusi, alisema kwa sasa umoja huo hauna mradi wowote unaoingiza mapato lakini kwa sasa wameandaa mpango kazi wa kuhakikisha wanakuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato.

Alisema katika eneo ambalo wanajenga nyumba za kupangisha lilikuwa ni ghala ambalo lilikuwa halitumiki na hivyo kwa muda mrefu lilikuwa haliwaingizii mapato yoyote.

Alisema waliamua kubadili matumizi na kuamua kujenga nyumba za kupangisha ambazo zitakuwa na vyumba 11 na kwamba malengo yao ni kupangisha kwa Sh. 50,000 kwa mwezi.

Alisema mbali na kujenga nyumba hizo za kupangisha pia wanaendelea na ujenzi wa nyumba ya kuishi ya Katibu wa UWT wa wilaya ili waondokane na adha ya kuishi kwenye nyumba ya kupanga.

"Tuliunda kamati ya manunuzi ambayo ndiyo inayoshughulikia ujenzi wa mradi huu kwa kuhakikisha mradi unakwenda kwa kasi, tunashukuru kwamba tunashikwa mkono na wadau mbalimbali," alisema Ruth.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole, alimshukuru Naibu Waziri Mahundi kwa kuendelea kuisaidia jumuiya hiyo kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema umoja huo utaendelea kumuunga mkono kwenye shughuli mbalimbali anazofanya zikiwamo za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maendeleo.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto), akishangiliwa na Umoja wa Wanawake Wajane nchini mwishoni mwa wiki baada ya kumaliza mkutano wa maandalizi ya kongamano la wajane kitaifa linalotarajiwa kufanyika mkoani Mbeya Juni 23, mwaka huu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## H'shauri Mbeya yatoa mil.15/- ujenzi matundu ya vyoo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imetoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vyenye matundu 20 katika Shule ya Sekondari Kalobe.

Hatua hiyo imekuja baada ya vyoo vilivyokuwa vinatumika awali kubomoka kutokana na mvuka kubwa iliyonyesha mwanzoni mwa mwaka huu.

Meya wa Jiji hilo, Dor-Mohamed Issa aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika shule hiyo kwa lengo la kuangalia maendeleo ya mradi huo ambapo aliwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wanautekeleza vizuri.

Alisema serikali imetoa fedha hizo ili kuwasaidia wanafunzi wa shule hiyo ambao wamekuwa wakihangaika baada ya vyoo vya awali kubomoka na kwamba yeyote atakayezitumia vibaya atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema mradi huo kwa sasa umefikia hatua ya kuezekwa na hivyo wanakusudia kupeleka fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha ili vianze kutumika mapema.

"Nimeridhika na kasi ya ujenzi wa vyoo hivi ambavyo ni vya watoto wetu wa kike, lakini nitoe angalizo kwa wasimamizi wasije wakacheza na fedha hizi, hapa tunategemea kuleta zingine kwa ajili ya umaliziaji na lazima zitumike kwa lengo hilo," alisema DorMohamed.

Alisema serikali inaboresha mazingira ya elimu kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu nchini na hivyo akawataka viongozi wa serikali walioko kwenye ngazi ya kata na mitaa kusimamia vizuri.

# TPA yaombwa kujenga kituo cha afya cha kisasa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya imeomba Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA) kujenga kituo cha afya cha kisasa katika Kijiji cha Kajunjumele kilichoko jirani na Bandari ya Itungi katika Ziwa Nyasa.

Kwa mujibu wa uongozi wa wilaya hiyo iwapo kituo hicho kitajengwa kitawezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa karibu kwa wananchi wa maeneo hayo pamoja na abiria wanaopata huduma na usafiri wa meli kupitia Bandari ya Itungi.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, aliyasema hayo wakati akipokea msaada wa vitanda 15 vya wagonjwa, magodoro 15 na meza uliotolewa na TPA kwa Halmashauri ya Wilaya hiyo ukiwa umegharimu Sh.milioni 33.7.

Manase alisema kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameona umuhimu wa kusogeza huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga na kuboresha miundombinu ya sekta hiyo ni muhimu na taasisi nyingine kuunga mkono juhudi hizo.

Hata hivyo alipongeza TPA kwa kuwa na mwenendo mzuri wa kurejesha sehemu ya faida wanayoipata kwa wananchi kwa kutoa misaada mbalimbali huku akisisitiza vitanda vilivyotolewa kupelekwa kwenye vituo vya afya vipya ambavyo bado kuna uhitaji.

Aliwasihi pia wananchi hususani wafanyabiashara kuzidi kuziamini huduma zinazotolewa na TPA na kutumia fursa za uwepo wa bandari katika Ziwa Nyasa kwa kusafirisha mizigo au wao wenyewe kusafiri.

"Rais amezipa msukumo mkubwa bandari zetu, huku kwetu tayari alitoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Ibanda hadi Banadi ya Itungi kwa kiwango cha lami... Hii ni kutokana na kutambua mchango na umuhimu wa bandari hii. Sasa kama rais anafanya hivyo kwa nini na sisi tusiunge mkono kwa kuzitumia bandari hizi," alisisitiza Manase.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Dk. Saumu Kumbisaga, alisema wilaya bado ina uhitaji mkubwa wa vifaa kwenye maeneo ya utoaji huduma za afya hivyo ni muhimu wadau zaidi kuendelea kujitolea.

Dk. Kumbisaga alisema ongezeko na mahitaji ya vifaa tiba wilayani hapa linatokana na nguvu ya serikali iliyowekezwa kwenye upanuzi wa sekta hiyo ikiwamo ujenzi wa vituo vipya vya kutolea huduma.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TPA, Plasduce Mbossa ambaye ni Meneja Uhusiano na Msoko wa Mamlaka hiyo, Nicodemus Mushi, alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwenye uboreshaji wa bandari nchini ndiyo unaipa nguvu TPA kupata faida na kuchangia kwenye maendeleo ya kijamii.

Alipongeza pia ushirikiano baina ya TPA na taasisi mbalimbali vikiwamo vyombo vya usalama akisema unaiwezesha mamlaka hiyo kufanya shughuli zake kwa weledi na kukidhi haja za wateja hasa kiusalama.

## ACT-Wazalendo yataka soko huria kilimo cha karafuu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kitaruhusu soko huria kwa karafuu punde watakaposhika madaraka baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Hayo yameelezwa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Othman Masoud Othman, wakati akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Jadida Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema mfumo unaotumika hivi sasa katika karafuu mkulima kufanyakazi ya kuzalisha na serikali kuuza katika soko la nje siyo mwafaka na unachangia kurudisha nyuma maendeleo ya zao hilo.

Alisema kwamba historia inaonesha Zanzibar ilikuwa inaongoza kwa zao la uzalishaji wa karafuu kwa kuzalisha karibu tani 20,000 lakini uzalishaji umeshuka na kufikia tani 4,000.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, alisema hakuna njia nyingine ya kuendeleza karafuu zaidi ya zao hilo kuachiwa kuwa huria jambo ambalo litamaliza hata biashara ya magendo.

Alisema: "Pamoja na serikali kufidia bei ya sasa kwa asilimia 80 wakulima bado kuna haja ya kuachiwa wenyewe wauze katika soko la nje badala ya wao kuwa wakulima na serikali kuwa wauzaji".

Alisema gharama za uzalishaji wa karafuu ni kubwa na kutoa mfano pishi moja linafaida ya Sh. 7,800 ukitoa malipo ya mchumaji na mkulima katika pishi moja mkulima anabakia na Sh. 4,000 mbali na gharama za matayarisho ya vifaa vya kukaushia karafuu.

Alisema karafuu daraja la kwanza hivi sasa inauzwa Sh.14,000 lakini serikali imekua ikilazimika kufidia bei kutokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia.

Akizungumzia wazalishaji wa mazao ya chakula, alisema wameshindwa kunufaika na soko la sekta ya utalii kwa sababu serikali imeshindwa kuwawezesha ili kuinua uzalishaji wa mazao mbalimbali.

"Sekta ya utalii Zanzibar inategemea chakula kutoka Tanzania Bara kwa sababu wakulima wetu hawakuandaliwa lakini kama wangewezeshwa leo wangeweza kunufaika na sekta hiyo," alisema.

Aidha, alisema asilimia 80 ya wafanyakazi katika sekta ya utalii wanatoka nje ya Zanzibar kwa sababu serikali haijawaandaa vijana wake kitaaluma tangu ilipoanzishwa sekta hiyo na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais mstaafu, DK. Salmini Amour Juma.

Othman alisema hatua hiyo inamadhara makubwa kwa sababu inasababisha mzunguko wa fedha Zanzibar kupungua na kusafirishwa nje ya Zanzibar wanakotoka wafanyakazi hao.

# Serikali yakazia sera utekelezaji wa diplomasia ya uchumi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema utekelezaji diplomasia ya uchumi ni miongoni mwa sera ya mambo ya nje ambayo serikali imeweka msisitizo.

Imesema hivi sasa kwa kushirikiana na wadau iko katika maandalizi ya mpango wa kitaifa wa uratibu, utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir.

Ameir alitaka kujua diplomasia mpya ya uchumi inachangia vipi kuleta mapinduzi ya viwanda na kilimo nchini.

Waziri Hamza alisema serikali kwa kushirikiana na wadau kutoka sekta za umma na binafsi imeendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuvutia uwekezaji, mitaji, elimu, masoko na teknolojia katika sekta mbalimbali zikiwamo za viwanda na kilimo.

"Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza diplomasia ya uchumi ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda na kilimo kufuatia ushirikiano wa kikanda na kimataifa," alisema.

Aidha, alisema hali hiyo imesababisha kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za Tanzania ikiwamo mazao ya kilimo nje ya nchi.

Alisema kwa mwaka 2022/2023 serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (SMT), wizara zinazosimamia elimu (SMZ na SMT), Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi (SMZ na SMT) iliwapeleka nchini Israel vijana 250 kwa ajili ya mafunzo ya utarajali wa kilimo na mifugo.

Waziri Hamza alisema uratibu wa kupeleka vijana wengine 260 unaendelea.



Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, akisoma mwongozo wa CAG kuomba radhi kwa kauli yake aliyoitoa kuhusu taarifa aliyoiwasilisha Ikulu hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matumizi bora ya ardhi bado ni tatizo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekiri kuwa licha ya jitihada za serikali katika kuimarisha matumizi bora ya ardhi nchini, bado kuna tatizo katika matumizi ya ardhi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Harusi Suleiman, katika kikao cha Baraza la Wawakilsihi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi.

Prof. Fakihi alitaka kujua serikali imetekeleza vipi mpango wa mazingira na hifadhi ya ardhi kuzuia mmong'onyoko wa ardhi na fukwe.

Akijibu swali hilo, Waziri Harusi alisema mambo yaliyofanywa na serikali kwa mwaka 2022/2023 ya kuzuia mmong'onyoko wa ardhi na fukwe ikiwa ni sehemu ya kutekeleza mkakati wa mabadiliko ya tabianchi wa Zanzibar wa mwaka 2014 ni kuanza ujenzi wa ukuta wa Sipwese, Wilaya ya Mkoani Pemba wenye urefu wa mita 320 ambao unajengwa kwa ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema pia imejenga tuta katika eneo la Tovuni, Wilaya ya Wete, Pemba lenye urefu wa mita 400 ili kuzuia mmong'onyoko wa fukwe.

Alisema juhudi zingine ni kujenga ukuta katika eneo la Msuka, Wilaya ya Michweni Pemba wenye urefu wa mita 500 na kujenga ukuta eneo la Kojani, Pemba wenye urefu wa mita 90.

Aidha, alisema serikali inasimamia utekelezaji wa mkakati wa kuvitumia visiwa vidogo kwa ajili ya uwekezaji ikiwa ni sehemu ya kudhibiti na kuvihifadhi visiwa hivyo.

"Hadi hivi sasa jumla ya visiwa vidogo vidogo 17 vimeshapewa wawekezaji kwa ajili ya kuviendeleza. Miongoni mwa masharti ya uwekezaji wa visiwa hivyo ni kulinda na kuhifadhi mazingira ya visiwa hivyo na bioanuwai zake pamoja na kuchukua hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema ni lazima kuweka mazingira mazuri katika ukodishaji wa visiwa hivyo ili kudhibiti athari za kimazingira.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (katikati) akiongoza semina ya wabunge kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 iliyofanyika jana katika Ukumbi wa Msekwa bungeni jijini Dodoma. Wa pili kushoto ni Spika mstaafu na Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, 2022, Anne Makinda. **PICHA: BUNGE**

# TAMWA yamlilia Leila

**Na Frank Monyo**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimempoteza aliyekuwa mwanzilishi na Mkurugenzi wa chama hicho kati ya mwaka 1996 hadi 2001, Leila Sheikh, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana jijini Dar es Salaam baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Leila alikuwa mwanahabari mkongwe na mtetezi wa haki za wanawake na watoto, aliyeongoza upatikanaji wa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA), wakati wa uongozi wake.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma, iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, Leila atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika tasnia ya habari na jinsia, tangu kuanzishwa kwa chama hicho miaka 30 iliyopita.

Alisema alikuwa mmoja wa waasisi wa TAMWA na alikuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya taifa katika mrengo wa jinsia na haki za wanawake na watoto kiujumla.

"Kabla ya kuwa Mkurugenzi wa TAMWA mwaka 1996, Leila alikuwa mhariri wa jarida la kwanza la haki za wanawake Tanzania-Sauti ya Siti mwaka 1989, akiwa amedhamiria kupaza sauti kupitia majarida kuhakikisha haki za wanawake zinafanyiwa kazi," alisema na kuongeza:

"Aliratibu timu ambazo zilishawishi Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA). Katika michakato yote hii, Leila alielewa maadili ya msingi ya mwanaharakati ambayo ni huruma, uelewa, kujitolea, ushirikishwaji unyenyekevu, ucheshi na amani," alisema Dk. Rose.

Alisema, Leila alikuwa ni mfano wenye nguvu kwa wakurugenzi wanawake kutokana na kazi aliyoifanya kama mwanaharakati, kuendesha shirika, kuhariri jarida la kitaifa na kuongoza mojawapo ya shughuli kubwa za wanaharakati ambazo ziliishia kupata sheria muhimu ya SOSPA.

"Alikuwa mwanablog mahiri na atakumbukwa kwa ubunifu wake, hasa baada ya kuanzisha mgahawa wa mtandaoni, aliouita; Leila's Cafe, akichambua masuala ya jinsia."

"Kwa kuwa alipenda zaidi kutambulika na kutekelezwa kwa haki za jinsia, Leila, alianzisha pia, kundi la facebook, lililoitwa Ustawi wa Jamii lililokuwa linajadili masuala ya jinsia pia," alisema Dk. Rose.

Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, alimzungumzia nguli huyo wa habari nchini kwa kusema: "Leila alikuwa mwalimu wa wengi kwenye harakati za usawa wa kijinsia na haki za binadamu, kupitia TAMWA alikuwa mstari wa mbele kuhakikisha jamii ya kitanzania inaheshimu na kuthamini usawa kwa watu wote."

"Leila alikuwa sio tu mwandishi mahiri pia alikuwa mtetezi wa wanawake, wasichana na watoto aliyetumia taaluma yake ya uandishi wa habari kwa ajili ya makundi haya," alisema.

Ofisa Habari TAMWA, Florence Majani alisema, Leila atakumbukwa kwa ukarimu wake kwa wanahabari, wakati wowote, alipotakiwa kuzungumzia masuala ya jinsia katika vyombo vya habari, alijitoa kwa hali na mali.

Mwasisi wa TAMWA, Rose Haji Mwalimu, alimwelezea Leila kuwa alikuwa ni mwanaharakati kindakindaki na 'Star' (nyota) ambaye alikuwa na maarifa mengi kuhusu masuala mbalimbali ya uandishi wa habari na jamii; alikuwa mbunifu; jasiri na hakuogopa kusimamia jambo lolote la kimaendeleo.

Leila alizaliwa Januari 8, 1958, mwili wake ulisafirishwa jana kuelekea Usagara, mkoani Tanga. Maziko yanayotarajiwa kufanyika makaburi ya Mabawa leo.

# CAG Zanzibar akubali yaishe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKAGUZI na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Zanzibar (CAG), Othman Abassi Ali, amewaomba radhi wajumbe Baraza la Wawakilishi kutokana na madai ya kuwakashifu wakati akiwasilisha ripoti yake ya mwaka 2022 mbele ya Rais.

Wiki iliyopita kuliibuka mjadala mkali kwa wajumbe wa baraza hilo akiwamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali kwa Mashirika ya Umma (PAC), Juma Ali Khatib, akimtaka CAG kuliomba radhi baraza hilo kutokana na kauli zake ambazo wamedai zinawadhalilisha.

Akitoa mwongozo jana kwa wajumbe wa baraza hilo, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, aliwataka wajumbe kuridhia msamaha huo wa CAG.

Alisema kwa kuheshimu Baraza la Wawakilishi, CAG Othman, alifika Juni 7 mwaka huu ofisini kwa Spika kueleza kauli alizozitoa na kuomba msamaha.

"Mdhibiti huyo kwanza anawaomba radhi sana wajumbe wote wa PAC, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC), Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na chombo chenyewe cha baraza, kwa maneno yake aliyoyatamka katika uwasilishwaji wa ripoti yake ambayo yeye mwenyewe alikiri kuwa hayaleti taswira nzuri kwa wajumbe na baraza kwa ujumla wake," alisema Spika Zuberi.

Pia mdhibiti huyo alisikitishwa na namna jamii ilivyompokea kwa kutafsiri na kuyapokea vibaya maneno yake hayo, na kuliomba baraza limsamehe kwa maneno yake na tafsiri iliyokuja baada yake.

Alisema pamoja na kuomba mwongozo ambao uliashiria kuombwa radhi hadharani, kwa kuzingatia kuwa mdhibiti huyo ameonyesha uungwana baada ya kuwakosea na kulikosea baraza, ndiyo maana alifika mwenyewe kuomba radhi.

Zuberi alisema mdhibiti huyo alikiri mbele yake kuwa hakukusudia kuonyesha dharau kwa maneno yake aliyoyatoa na kwa kuwa yeye pia ni sehemu ya Kamati za PAC na LAAC za baraza na kwamba anafanya kazi kwa karibu na baraza hilo tukufu.

"Waheshimiwa wajumbe, mwongozo wangu wa suala hili ni kukubaliana na ninyi waheshimiwa mlioomba mwongozo huo kuwa maneno aliyotoa mdhibiti hayakuwa mazuri kwa kamati na baraza kwa ujumla," alisema.

"Lakini kwa kuwa amekiri makosa yake na alikuja mwenyewe na kuomba radhi, hivyo ninaelekeza kuwa suala hili limalizike hapa na kwa kuzingatia Kanuni ya 64(6) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ninaomba kutoa mwongozo wangu huu na kusitisha mjadala wowote juu ya suala hili."

Juni 5, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, Juma Ali Khatib, alisimama na kuomba mwongozo wa Spika chini ya kanuni ya 64(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, kutokana na kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, aliyoitoa wakati anawasilisha ripoti za ukaguzi mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Juni 3, mwaka huu katika viwanja vya Ikulu Zanzibar.

Kwa mujibu wa ombi hilo, Juma amehisi kuwa kauli ya mdhibiti huyo kuwa PAC na LAAC hazina uwezo wa kuzifanyia kazi ripoti zake ikiwamo ya TEHAMA, ilitafsiriwa ni kulibeza na kulidharau Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Juma aliendelea kueleza kuwa kauli hizo zinakwenda kinyume na kanuni ya 46 ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria ya Kinga Uwezo na Fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Namba 6 ya 2022 na Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi Namba 6 ya mwaka 2019, kwa pamoja zinaheshimu haki, fursa na uwezo wa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wa Baraza hilo.

Pia alionesha athari ya kauli hizo kuwa zimepokelewa vibaya na jamii ya Zanzibar na hasa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha kuwa Baraza la Wawakilishi na kamati zake, hazina uwezo wa kufanya kazi zao hasa katika eneo la usimamizi wa fedha za umma.

"Kauli hizo za mdhibiti zinaonyesha wazi kuwa wajumbe wa kamati za kudumu za baraza hasa walioteuliwa kutekeleza kazi za kamati ya PAC na LAAC, ni 'vilaza' na wamekosa uwezo na utayari wa kutekeleza majukumu yao ya kikatiba na kisheria."

Wajumbe wa baraza hilo waliridhia kitendo alichokifanya CAG cha kuomba radhi.


## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

**Asofu Ndugu Alfred Juma** Okeyo wa Kanisa la Evangelical Pentecostal Restoration Church (EPRC) anatangaza kupotelewa na cheti cha usajili wa Kanisa chenye namba **S.A.22244** kilichotolewa **9/9/2021.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.


Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/190346/2023**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED, I KIBIBI SHABANI MHINA** a citizen of Tanzania, **DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name of **KIBIBI SINJE** as it can be seen in my Parastatals Pension Fund and adopt as from the date of this need poll and in substitution of my former name, the name of **KIBIBI SHABANI MHINA** as it appears in my National Identity Card **No. 19540513-61202-00001-19.** For the purpose of evidence of such determination, I, hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever us and subscribe the said name of **KIBIBI SHABANI MHINA** as my name in lieu and in substitution for my former name of **KIBIBI SINJE.**

**AND I HEREBY** expressly authorized and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **KIBIBI SHABANI MHINA.**

**IN WITNESS WHEREOF** I have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old name of **KIBIBI SINJE** by my new name of **KIBIBI SHABANI MHINA.**




**MIJNET COMPANY LIMITED**
**AUCTION MART MOROGORO**
**S.L.P. 1983**
**MOROGORO - 08/06/2023**

## TANGAZO LA MNADA

KWA NIABA YA NEEMA GROUP TUNAUZA DHAMANA YA NAPOLEON ELEUTER DALU KAMA DHAMANA YAKE YA MKOPO ALIYOKOPA. DHAMANA YENYEWE NI NYUMBA YENYE CHUMBA NA SEBULE. UKUBWA WA KIWANJA KWA UREFU 44&35 NA UPANA 35&26 NAMBA YA NYUMBA NI 1179 KILICHOPO MTAA WA KOROGOSHO KATA YA BIGWA MANISPAA YA MOROGORO.

MNADA UTAFANYIKA TAREHE 17/06/2023, SAA 4;00 ASUBUHI SIKU YA JUMAMOSI FIKA MAPEMA UKAKAGUE ENEO HUSIKA.

WASILIANA NASI UKAKAGUE KABLA YA MNADA AU MUONE MWENYEKITI WA MTAA WA KOROGOSHO ATAKUONYESHA NYUMBA ILIPO

**MAWASILIANO: 0714 557 680**
**0652 684 325**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**NICHOLAUS SIXTUS TOKE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3470/0075** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ABBEY SEKONDARI** mwaka **2016.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/196288/2023.**

## Moro kupanda michikichi 500,000

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imeazimia kupanda miche 500,000 ya michikichi ya mbegu za kisasa itakayobadilisha uchumi kwa kiasi kikubwa kuanzia mwaka 2023 hadi 2030 kwa kuzalisha tani mil. 3 za malighafi na kuwa moja ya mikoa yenye uzalishaji mkubwa wa zao hilo nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliyasema hayo jana alipotembelea shamba la mbegu za Michikichi Msimba linalosimamiwa na wakala wa mbegu (ASA) lenye miche zaidi ya 170,000 lililopo katika kitongoji cha Msimba wilayani Kilosa mkoani hapa.

Alisema miche hiyo 500,000 itapandwa katika wilaya tano ambazo ni Kilosa, Kilombero, Mlimba, Malinyi na Ulanga kwa sababu wananchi wake wameonesha nia ya kupanda michikichi ya asili isiyowapa tija inayotakiwa.

Alisema matarajio ya mkoa ni kwamba hadi kufikia mwaka 2030 wakati Rais Samia Suluhu Hassan anamaliza kipindi chake cha pili cha uongozi mkoa wa Morogoro uwe na michikichi zaidi ya milioni 1 inayozalisha kama tani milioni 3 za malighafi ya michikichi.

Alisema Mkoa wa Morogoro kwa sasa una jumla ya watu milioni 3.4 na wakati watu wakifika milioni 4.5 au 5 anataka uzalishaji wa kiuchumi uwe umeongezeka sana katika mazao mbalimbali ikiwamo mkonge, miwa, michikichi na mpunga.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo, Dk. Sophia Kashenge, alisema kilimo cha michikichi kinaendelezwa katika vitalu kwa kutumia umwagiliaji ambapo mche mmoja unatumia miezi 12 hadi 18 kitaluni, ili usife baada ya kupandwa shambani ambao unatumia gharama ya Sh. 2,800 hadi 3,000.

Akizungumzia faida za michikichi ya kisasa Dk. Kashenge alisema mche mmoja wa kisasa hutoa tani 3- 5 za michikichi zenye ujazo zaidi kwa miaka 2 hadi miwili na nusu ya ukuaji hadi uvunaji tofauti na mti wa asili wenye kutoa chini ya tani 1 kwa mti mmoja wa mchikichi.

# TPDC yatumia bil. 2/- kutekeleza miradi ya kijamii inakopita gesi

**Na Gwamaka Alipipi,** aliyekuwa MTWARA

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limetumia zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa miaka mitano kutekeleza miradi ya huduma za jamii katika maeneo ambayo miradi ya gesi asilia imesimikiwa na kupita.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa TPDC, Marie Msellem, alibainisha hayo katika ziara ya waandishi wa habari walipotembelea miundombinu ya bomba la gesi asilia mikoa ya Lindi na Mtwara.

Ziara hiyo ilihusisha kutembelea kiwanda cha uchakataji gesi asilia cha Madimba na visima vya kuchakata gesi vya Mnazi Bay mkoani Mtwara na Somanga.

Marie alisema: "Wananchi waliopo vijiji vya pembezoni mwa mradi kwanza wanalipwa fedha za kufanya ulinzi na kusafisha, kuondoa vichaka na hatari zozote.

"Wananchi wakiona sehemu udongo umeporomoka na bomba linaonekana wanatoa taarifa TPDC. Pia katika kurudisha tunalipa fedha inawezekana isitoshe, lakini tunafanya uwajibikaji kwa kuwa tunarudisha kidogo kwa jamii ambao wao ndiyo walinzi wa bomba na ni kipaumbele chetu".

Marie alisema TPDC imejenga shule, madarasa, zahanati, wodi za kinamama na mtoto, visima vya maji, vyoo na vitu vingi vya huduma za kijamii katika vijiji 139 ambavyo bomba la gesi limepita.

Marie alibainisha gesi asilia inatumika kwa matumizi mbalimbali ikiwamo uzalishaji umeme, hivyo asilimia 60 ya umeme wa Tanzania unategemea gesi asilia.

Alisema nishati hiyo tayari imewafikia wananchi 2,000 majumbani na magari zaidi ya 2,000 yameunganishwa na mfumo wa gesi asilia.

Marie alisema wananchi waliounganishwa na gesi hiyo ni wakazi wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam.

Awali, waandishi hao walitembelea visiwa vya kuzalisha gesi asilia vya Mnazi bay, ambapo Msimamizi wa Uzalishaji gesi wa Kampuni ya Maurel & Prom Tanzania (MP), Hussein Chitemo, alieleza wana visima vitano vya kuzalisha gesi asilia.

Chitembo alisema gesi inayozalishwa Mnazi Bay inakusanywa, kuichakata na kisha kuipeleka kwa wateja wao ambao ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mtwara wanayoitumia kuzalisha umeme kwa mikoa ya kusini.

Alisema mteja mwingine ni TPDC kupitia kampuni tanzu yake ya GASCO, kwamba gesi hiyo huipeleka katika kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba.

Chitemo alisema uzalishaji wa gesi asilia ulianza mwaka 2015 na kwamba visima vyote vitano vinazalisha gesi asilia futi za ujazo milioni 110.

Alisema gesi asilia ina faida nyingi ikiwamo kuzalisha umeme na matumizi ya viwandani.



Makamu wa rais wa kiwanda cha kuzalisha pikipiki aina ya TVS kilichoko India, Rahul Naik, akikata utepe kuzindua duka jipya la spea za bidhaa hiyo, Kariakoo jijini Dar es Salaam juzi. Alisema kuwa litakuwa msaada kwa mawakala walioko hapo na maeneo mengine kupata spea kiurahisi. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Wabunifu kidijitali 'kupikwa' kwa wiki mbili

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeianza safari ya wiki mbili ya kuwapika wabunifu 196 waliochaguliwa katika programu yake ya Imbeju inayolenga kutoa mtaji wezeshi kwa vijana na wanawake.

Washiriki hao ni kati ya wabunifu 709 waliotuma maombi yao kuanzia Machi 12 programu hiyo ilipozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kukidhi vigezo vya awali vilivyowekwa.

Akifungua mafunzo hayo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, aliwapongeza washiriki waliofanikiwa kufika hatua hiyo, akiwasisitiza kuwa ubunifu wao wa kipekee, shauku yao isiyoyumba na jitihada zao katika ujasiriamali zimewaweka mbele ya kundi kubwa la washiriki waliowasilisha maombi yao, hivyo kuwa sehemu ya fursa hiyo.

"Tunapoianza kambi hii ya mafunzo, ni wakati muhimu katika safari yenu ya ujasiriamali kwani mtapata fursa ya kuboresha bidhaa na huduma zenu, mikakati na kupata ujuzi muhimu unaohitajika ili kuwawezesha kufanikiwa katika hatua hii ya mwanzo katika uendeshaji wa biashara.

"Niwasihi kujifunza kwa umakini mkubwa ili kutumia mafunzo na uzoefu mtakaoupata kuboresha biashara zenu. Kumbukeni kuwa maarifa ni nguvu na kwa kujijengea ufahamu na ujuzi sahihi, mtakuwa tayari kukabiliana na changamoto na kuchukua fursa nyingi zilizopo mbele yenu. Na hapo ndipo mafanikio ya programu hii yatakapoonekana," alisema Nsekela.

Mkurugenzi huyo pia alisisitiza dhamira isiyoyumba ya Benki ya CRDB kusaidia kukuza biashara changa nchini kupitia mitaji wezeshi hasa zile zinazomilikiwa na vijana na wanawake, makundi muhimu yasiyopewa kipaumbele katika fursa za uchumi.

Nsekela alisisitiza kuwa Benki ya CRDB inaelewa kuwa upatikanaji wa fedha ni jambo muhimu katika kubadilisha mawazo bunifu kuwa biashara endelevu, hivyo programu ya Imbeju inalenga kuchochea mafanikio ya wabunifu na waanzilishi wa biashara na kuhakikisha fedha haiwi kikwazo cha safari yao ya ujasiriamali.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa, alisema wanatambua kuwa mtaji si kikwazo pekee cha vijana wenye mawazo bunifu kuyageuza kuwa biashara inayotatua changamoto za jamii kwa kuwa takwimu zinaonyesha biashara nyingi changa zimekufa si kwa sababu ya mtaji, bali kutokana na kukosa maarifa sahihi ya usimamizi na uendeshaji wa biashara.

"Leo tupo hapa kutekeleza kile tulichoahidi kwa maana ya kutoa mafunzo yanayolenga kuwaongezea uwezo vijana walioomba mtaji wezeshi wa Imbeju ili ikifika hatua ya kuwawezesha kwa mtaji, wawe tayari kutumia mtaji huo kwa ufanisi na kuleta matunda yaliyokusudiwa," alisema Tully.

Programu ya Imbeju inatekelezwa katika madirisha mawili; la kwanza ni la ushindani linaloshindanisha miradi ya ubunifu itakayopewa mtaji wezeshi ambalo linaendeshwa kwa ushirikiano na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Tume ya TEHAMA (ICTC) ikiwalenga vijana na wanawake.

Dirisha la pili ni mahsusi kwa wanawake hasa waliopo katika vikundi. Tangu kuzinduliwa kwa programu ya Imbeju mpaka Mei 31, dirisha hilo limetoa mafunzo kwa vikundi vya wanawake 1,341 vyenye wanachama 18,614 nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema vijana wengi wanaamini mtaji ni fedha tu bila kufahamu kuwa hata wazo pekee ni mtaji ambao mwenye nalo akishikwa mkono anaweza kulifanya biashara kwa kutatua kero iliyopo katika jamii.

Mkurugenzi Mkuu wa ICTC, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema ICTC ina kazi kuu mbili - kuratibu kazi na shughuli za TEHAMA nchini na kutekeleza sera ya Taifa ya TEHAMA.

# NAMUNGO KUJITATHMINI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Namungo kesho unatarajia kukutana kupitia ripoti ya msimu wa Ligi Kuu uliomalizika wiki iliyopita na kufanya tathmini kabla ya kuanza maandalizi ya msimu ujao wa ligi.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Ally Selemani, alisema kuwa kamati ya utendaji itakutana kesho kuweka mikakati kwa ajili ya msimu mpya wa 2023/2024.

**"Hatuwezi kuanza mipango ya msimu ujao kabla hatujapitia ripoti ya msimu huu na kuifanyia tathmini, kikao cha Jumatano (kesho) ni muhimu sana na ndio kitatupa dira ya mikakati yetu kuelekea msimu ujao wa ligi," alisema Selemani.**

Alisema msimu huu ulioisha hawakufikia malengo waliyojiwekea ikiwamo kurejea tena katika mashindano ya kimataifa kama ilivyokuwa misimu miwili iliyopita ambapo walicheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Aidha, Katibu huyo alitoa ufafanuzi juu ya tetesi zinazohusisha klabu hiyo kutaka kumchukua kocha wa zamani wa Kagera Sugar Patrick Odhiambo ili kuifundisha timu hiyo ya mkoani Lindi msimu ujao.

"Tunahitaji kufanya maboresho ya kikosi kulingana na mahitaji ya timu kuhusu suala la kocha hilo ni mapema mno kulizungumzia kwa sababu bado uongozi hatujakutana, tukikutana na kuweka mikakati yetu ndio tunaweza kuzungumzia masuala yote ya namna gani tutakiimarisha kikosi chetu," alisema Selemani.

Alisema wamenatarajia kufanya maboresho mazuri ya kikosi cha timu yao kwa kufanya usajili wa nyota wenye kiwango bora kwa ajili ya kupambania timu hiyo kurejea katika michuano ya kimataifa mwakani.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Muza, wakifanya mazoezi ya mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mukadi: Nakuja kupiga mtu Tanzania

**Na Saada Akida**

BONDIA Erick Mukadi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, amesema anajiandaa vizuri kwa ajili ya pambano lake la Juni 30 dhidi ya Mtanzania Seman Kidunda na anakuja Tanzania kufuata ushindi kwa kumpiga mpinzani wake.

Mukadi ametoa kauli hiyo kuelekea katika pambano hilo lililoandaliwa na Kampuni ya PAF Promotion Company Limited huku likipewa jina la 'Hata usipolala Patakucha tu' ambapo pia Mfaume Mfaume atapanda ulingongi dhidi ya Nkululeko Mhlongo wa Afrika Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mukadi alisema anakuja Tanzania kwa kazi ya kuhakikisha anampiga vibaya Seleman Kidunda kutokana na maandalizi makubwa ambayo anaendelea kufanya.

"Nipo sawa naendelea na maandalizi yangu kwa ajili ya pambano langu na Kidunda, ninachotaka kumwambia kuwa nakuja Tanzania kumpiga Kidunda, tena nitampiga vibaya sana na kumfundisha ngumi," alisema Mukadi.

Alisema Tanzania ikae tayari kwa sababu anakuja kufanya kitu kibaya kwa bondia wake na anafanya maandalizi makali ya kutoa kipigo na kutoa onyo kwa mabondia wengine wa Tanzania.

Siku hiyo ya Juni 30 kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi ambapo bondia Fadhili Majiha 'Stopper' atapanda ulingoni kupigana na Jamal Kunoga, Saleh Kasim atapigana na Said Bwanga na Deo Samweli atapigana na Adam Ngange.

Mapambano mengine Pius Mpenda atapanda ulingoni dhidi ya Simon Tichecha wa Malawi wakati Rama John Cena akitarajia kupigana na Yona Segu, Omary Maulid atapanda ulingoni kupigana na Shaban Kibiriti, Boniface Seguda atapigana na Hamza Mahamoudu wakati Herry Rashid akitarajia kupigana na Hussein Pendeza.




## Kipanga FC yajipanga Z'bar

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa timu ya Kipanga FC ya Zanzibar, Hamis Hassan amesema atafanya usajili wa uhakika na wa kishindo kwa ajili ya kuiboresha timu hiyo kuelekea kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar inayotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Alisema anaiandaa timu yake ili kuhakikisha msimu ujao inafanya vizuri na kufikia malengo yao.

"Nataka kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani kwenye timu yangu msimu ujao, naomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono na hatutawaangusha msimu ujao," alisema Hassan.

Kocha huyo alisema katika usajili wake atawekeza nguvu kwenye safu ya ulinzi na ushambuliaji ambazo ameona hazikufanya vizuri msimu uliopita.

"Wapo wachezaji ambao nimeanza kuwafikiria kuwaongeza katika nafasi ya mshambuliaji na beki, naamini nitawapata na kukiboresha kikosi changu," alisema Hassan.

Aidha, alisema kwenye kikosi alichonacho sasa wapo wachezaji ameshauri waongezewe mikataba yao na wapo ambao watawaacha.

## Mchezo wa bao kushiriki maonyesho Sabasaba

**Na Abdallah Mataka**

SHIRIKISHO la Mchezo wa Bao nchini (SHIMBATA) limesema linajiandaa kushirikia kwenye maonyesho ya kimataifa ya biashara (Sabasaba) mwaka huu ili kutoa fursa kwa wachezaji, mashabiki na wadau wa mchezo huo kupata nafasi ya kuucheza, kuangalia na kujifunza mchezo huo.

Akizungumza na Nipashe, Rais SHIMBATA, Mandai Likwepa, alisema wameamua kufanya hivyo ili kuuinua na kuutangaza mchezo huo wa asili.

Alisema mchezo huo wa bao kuwepo kwenye maonyesho hayo kutaufanya kujulikana zaidi kwa baadhi ya watu.

"Katika maonyesho ya biashara ya Sabasaba wanakuja wageni kutoka katika mataifa mbalimbali hivyo wakiuona na kujifunza huu mchezo itakuwa fursa kwetu kuutangaza mchezo wa bao kimataifa pia," alisema Likwepa.

Aidha, Likwepa ameongeza kuwa wanafanya jitihada kuhakikisha mchezo huo unakuwapo katika maadhimisho ya kilele cha mbio za Mwenge kitaifa kwa lengo la kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ambaye alikuwa akiucheza mchezo huo enzi za uhai wake, kilele cha mbio hizo za Mwenge kitaifa zitafanyika Mkoa wa Manyara.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEYMAR NA WAARABU

WAWAKILISHI wa klabu ya Al-Hilal ya Saudi Arabia wako mjini Paris kujaribu kupata saini ya fowadi wa Paris St-Germain na Brazil, Neyma, 31. ***(CBS)***

### ONANA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA iko tayari kuwapa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku,30 na mlinzi wa Senegal, Kalidou Koulibaly, 31, Inter Milan katika jitihada za kumnunua kipa Andre Onana mwenye miaka 27. ***(Sun)***

### MADDISON AWANIWA

KLABU ya Newcastle United inaongoza dhidi ya Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo mshambuliaji wa Leicester City, James Maddison, 26, mwenye thamani ya pauni milioni 40. ***(Sky Sports)***

### SPURS YAMTAKA RAYA

TOTTENHAM Hotspur inakaribia kuafikiana na mlinda mlango wa kimataifa wa Hispania anayeicheza Brentford, David Raya, 27, ambaye analengwa na Manchester United. ***(Fabrizio Romano via Goal.com)***

### ZAHA AWINDWA NA PSG

WINGA wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha, 30, yuko kwenye mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu uhamisho wa bila malipo kwa mabingwa hao wa Ufaransa mara tu mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto. ***(Sun)***

### MOURINHO ATAKIWA ARABUNI

KLABU ya Saudi Arabia Al-Hilal inamtaka kocha wa zamani wa AS Roma, Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur, Jose Mourinho kuwa kocha wao mpya. ***(Mercato)***

### JAMES AKARIBIA LIVER

LIVERPOOL inakaribia kumnunua kiungo wa kati wa Southampton na England, James Ward-Prowse, 28, baada ya kuonekana kushindwa kumpata kiungo wa kati wa Chelsea, Mason Mount, 24, ambaye anatazamiwa kujiunga na Manchester United. ***(Mirror)***

### MUANI AWANIWA

NYOTA wa Eintracht Frankfurt, Randal Kolo, 24 ni miongoni mwa washambuliaji sita ambao Manchester United wanaye kwenye orodha yao fupi, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anataka kuhakikishiwa kuwa atakuwa kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Erik ten Hag. ***(Manchester Evening News)***

### THURAM NA LIVERPOOL

LIVERPOOL tayari ipo kwenye mazungumzo ya awali na kiungo wa Nice, Khephren Thuram, 22. ***(Football Insider)***

### RICE NA ARSENAL

UHAMISHO wa kwenda Arsenal wa kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice utakuwa wa mkataba kwa muda mrefu. ***(Mail)***

### GERRARD ATAKIWA SAUDIA

KOCHA wa zamani wa Rangers na Aston Villa, Steven Gerrard, 43, anafikiria ofa ya kuwa kocha wa klabu ya Al-Ettifaq ya Saudi Arabia, ambayo ina nia ya kumpata nahodha huyo wa zamani wa Liverpool. ***(Reuters)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BELLINGHAM ATEMWA ENGLAND MECHI ZA KUFUZU EURO 2024

**LONDON,** England

●●● Wote wanajiweka katika hali nzuri lakini hatufanyi mazoezi na timu katika kipindi...

JUDE Bellingham na Lewis Dunk wameondolewa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England kwa ajili ya mechi za kufuzu Euro 2024 dhidi ya Malta na Macedonia Kaskazini.

**Bellingham aliyesajiliwa na Real Madrid bado anauguza jeraha la msuli wa paja ambalo lilimweka nje kwenye mechi ya mwisho ya Borussia Dortmund, waliposhindwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, baada ya sare ya 2-2 nyumbani na Mainz.**

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 19 ataripoti St George's Park ili kupata matibabu zaidi, lakini hatacheza mechi yoyote, taarifa ya timu ilithibitisha.

Beki wa Brighton, Dunk amejiondoa kwenye kikosi kutokana na jeraha na hatasafiri katika kituo cha taifa cha soka - mchezaji pekee kutoka kikosi cha awali cha wachezaji 25 cha kocha Gareth Southgate ambaye kwa sasa hatastahili kujiunga.

Wachezaji wa England walianza kukusanyika pale St George's Park Jumapili, wakijiandaa kwa safari ya Ijumaa kucheza na Malta huko Ta' Qali na mechi ya Jumatatu dhidi ya Macedonia Kaskazini kwenye uwanja wa Old Trafford.

Declan Rice wa West Ham, ambaye alinyakua taji la Ligi ya Europa Conference katikati ya wiki, atajiunga siku zijazo, kama vile wachezaji watano wa kikosi cha Manchester City walioshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Jack Grealish, John Stones, Phil Foden, Kyle Walker na Kalvin Phillips wote jana Jumatatu walikuwa sehemu ya gwaride la mabasi ya City mjini Manchester kabla ya kuripoti kambini.

Katika video iliyotumwa kwenye akaunti za mitandao ya kijamii ya timu ya taifa ya England Jumapili, Southgate alisema: "Tuna mazoezi machache kidogo na tunasubiri wachezaji wote kuja.

"Wote wanajiweka katika hali nzuri lakini hatufanyi mazoezi na timu katika kipindi hicho na lazima urekebishe mwili wako.

"Nadhani tulichoonyesha katika miezi michache iliyopita ni kwamba sisi ni timu ambayo sasa inaweza kuwa timu bora zaidi duniani.

"Tulionyesha hilo kwenye Kombe la Dunia na kwa hakika tulionesha hilo kwa kushinda kwa Naples (ushindi wa 2-1 dhidi ya Italia Machi), ambao ulikuwa mchezo muhimu kwetu sio tu katika suala la kufuzu lakini kwa kujiamini na kuweka alama fulani kwa kile tulichonacho kama timu.

# TEN HAG: LINDELOF HAONDOKI MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa klabu ya Manchester United, Erik Ten Hag amesema kuwa beki wake raia wa kimataifa wa Sweden, Victor Lindelof hauzwi na yupo kwenye mipango yake ya muda mrefu ndani ya timu hiyo.

Ten Hag yupo tayari kumwachia beki wake raia wa England, Harry Maguire lakini si Lindelof ambaye amekuwa kwenye kiwango bora hasa katika michezo ya mwishoni kitu kilichomfanya kocha kumwamini na kuhitaji kuendelea kuwa naye kikosini.

Klabu za Inter Milan na Frankfurk ziliulizia huduma ya beki huyo katika dirisha dogo la Januari.

Lakini Man United hawakuwa tayari kumwachia beki huyo na klabu hizo zimerudi tena dirisha hili lakini kocha wa klabu hiyo hayuko tayari kumwachia.

Ten Hag yuko kwenye mpango wa kuitengeneza timu hiyo kwa muda mrefu na kuirudisha kwenye mafanikio kama miaka ya nyuma, hivyo anahitaji kubakiza wachezaji wake muhimu kwenye kikosi na moja ya wachezaji hao ni Lindelof.

Mwanzoni mwa msimu ilionekana kama Lindelof hatakuwa na muda mrefu ndani ya timu hiyo kutokana na ufinyu wa nafasi ambao alikuwa anaupata, lakini imekuwa tofauti kwani kocha alimwamini beki huyo kwa kumpa nafasi na yeye ameweza kulipa vizuri fadhila kwa kuonesha kiwango bora.

# Rodri mchezaji bora wa Ligi ya Mabingwa

**MANCHESTER,** England

MFUNGAJI wa bao pekee na la ushindi wa Manchester City, Rodri amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa msimu na Shirikisho la soka Ulaya, UEFA.

Wachezaji saba wa Man City wametajwa kwenye timu bora ya msimu na Erling Haaland akitwaa tuzo ya bao bora la msimu.

Bao la Rodri dakika ya 68 lilifanya tofauti wakati City ilipoilaza Inter Milan 1-0 mjini Istanbul nchini Uturuki Jumamosi na kubeba Kombe la Ulaya na kukamilisha msimu kwa mataji matatu.

Na Jumapili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alitawazwa mchezaji bora wa msimu na jopo la waangalizi wa kiufundi la UEFA.

Rodri alicheza katika mechi zote isipokuwa moja ya Ligi ya Mabingwa ya City msimu huu, huku Jumamosi akifunga bao lake la pili katika mashindano hayo.

Kiungo huyo wa kati wa Hispania alijumuishwa na wachezaji wenzake sita katika timu ya msimu huu ambao ni Haaland, Kevin De Bruyne, John Stones, Ruben Dias, Bernardo Silva na Kyle Walker.

Federico Dimarco wa Inter na Alessandro Bastoni pia walichaguliwa pamoja na kipa wa Real Madrid, Thibaut Courtois na fowadi Vinicius Junior.

City pia ilinyakua tuzo ya bao bora la msimu kupitia kwa Haaland kwa bao lake la sarakasi dhidi ya klabu ya zamani ya Borussia Dortmund wakati wa hatua ya makundi, alipopinda na kugeuza pasi ya Joao Cancelo na kutinga wavuni wakati City iliposhinda 2-1.







# *Sancho anafukuziwa na Tottenham Spurs*

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspurs imeripotiwa kumfukuzia winga wa klabu ya Manchester United, Jadon Sancho katika dirisha hili la usajili ili kuboresha kikosi chao.

Sancho ambaye alijiunga na Man United mwaka 2021 anahitajika na klabu hiyo kutoka kaskazini mwa jiji la London ili kuhakikisha wanarudi kwenye ubora wao baada ya kuwa na msimu mbovu wa 2022/23.

Man United inaripotiwa kuhitaji kiasi cha euro milioni 60 ili kumuachia winga huyo wa kimataifa wa England.

Kama Tottenham watakubali kutoa kiasi hicho cha fedha ni wazi mchezaji huyo ataelekea Spurs msimu ujao.

Sancho tangu ajiunge ndani Man United amekua na kiwango cha kusuasua kitu ambacho kimefanya klabu hiyo kufikiria kumuuza kwani ni msimu wa pili sasa hajafanikiwa kuonesha ubora ambao alikuwa nao ndani ya Borussia Dortmund.

Man United ina mpango wa kuondoa wachezaji kadhaa klabuni hapo kuelekea dirisha hili kubwa ili waweze kusajili wachezaji wengine wenye ubora mkubwa.

Huku Jadon Sancho akiwa kwenye orodha hiyo hivyo klabu ambayo itafika bei wanayoitaka United mchezaji huyo atauzwa Spurs nao wakiwa ndio wako mstari wa mbele.

# KMC, Mbeya City zapigania uhai Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu ya Green Warriors ya Dar es Salaam ikifanikiwa kusalia ligi daraja la kwanza 'Championship', timu za Mbeya City na KMC zinakutana leo kwenye mechi ya mchujo 'play off' kusaka timu itakayosalia Ligi Kuu kwa msimu ujao.

Maafande wa Green Warriors, ambao walifanya vibaya kwenye ligi ya Championship kiasi cha kucheza 'play off' dhidi ya Dar City, timu ya Ligi Daraja la Pili 'first leugue', juzi ilipata ushindi mnono wa mabao 4-1 kwenye mchezo uliochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Matokeo hayo yanaifanya timu hiyo kupata ushindi wa jumla wa mabao 5-2 baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa Juni 4 kwenye uwanja huo huo, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

Kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, timu ya Mbeya City leo itakuwa mwenyeji wa KMC katika mechi ya kwanza ya mchujo, kusaka timu itakayosalia Ligi Kuu na itakayoshuka daraja kwenda Championship.

Ijumaa iliyopita, timu hizo zilicheza mechi ya mwisho ya Ligi Kuu, Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga, KMC ikishinda bao 1-0.

Matokeo hayo yalizifanya kushika nafasi ya 13 na 14, hivyo kulazimika kwenda kucheza mechi ya mchujo.

KMC ilishika nafasi ya 13 na pointi 32, Mbeya City nafasi ya 14 ikiwa na pointi 31.

Mechi ya marudiano inatarajiwa kuchezwa Ijumaa ijayo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, siku ambayo mbivu na mbichi zitajulikana hapo.

# Simba yawatoa hofu mashabiki

INATOKA UKURASA 24

sifa ya kuichezea Simba lakini wapinzani wetu wanawahusisha na sisi (Simba), lengo ni kuwavuruga mashabiki na wanachama wetu, niwaombe msifuatilie taarifa za kwenye mtandao, taarifa sahihi zitatolewa na klabu kwenye 'Platfomu' zetu," alisema Ally.

Alisema kinapokuja kipindi cha usajili kuna mikakati mingi ikiwa pamoja na kuwatangaza wachezaji ambapo mameneja wa wachezaji hao wanatumia klabu kubwa kama Simba kuwatangaza wachezaji wao hata kama Simba haina mpango nao.

"Yaani mchezaji Simba hatuna mpango naye, lakini unasikia tunamtaka, viongozi wamezungumza naye, au wamemsafirisha, halafu inakuja kuibuka taarifa kuwa mchezaji amechukuliwa na klabu nyingine na hii inafanywa makusudi ili mashabiki waone wamepokonywa mchezaji na lawama zielekezwe kwa viongozi wetu, mashabiki wetu watulie taarifa kamili kwa kila mchezaji tunayemtaka na kumsajili watazipata kupitia kwa viongozi na Platfomu zetu," alisema Ally.

Uongozi wa Simba kwa sasa upo kwenye mchakato wa kuimarisha kikosi chao uku wakiweka wazi kufanya usajili kutokana na matakwa ya Kocha wao, Robert Oliviera 'Robertino'.

# SIMBA YAPIGA HESABU KUMRUDISHA KOCHA WAO




**Na Saada Akida**

KATIKA kujipanga na kujiimarisha kwa ajili ya msimu ujao, inaelezwa uongozi wa Simba umeanza mchakato wa kumrejesha kikosini kocha wao wa zamani wa magolikipa, Milton Nienov ambaye kwa sasa ni kipa wa makipa wa Yanga.

Taarifa kutoka ndani ya Simba zinadai kuwa viongozi wa Simba wameshakubaliana kila kitu na kocha huyo na walikuwa wanasubiri Yanga icheze mchezo wake wa fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) dhidi ya Azam FC (jana).

**Mmoja wa viongozi wa Simba aliiambia Nipashe kuwa kocha huyo raia wa Serbia amemaliza mkataba wake ndani ya Yanga na tayari wameshafanya naye mazungumzo.**

"Ni kweli kuna maboresho makubwa ya benchi la ufundi yatafanyika, wapo ambao wataachwa na kuongezwa wapya watakaokuja kushirikiana na kocha wetu mkuu Robert Oliveira (Robertinho) ambaye amewapendekeza kuja kufanya nao kazi," alisema kiongozi huyo.

Alisema kuchukuliwa kwa Nienov kunatokana na mahitaji ya timu baada ya kuachana na aliyekuwa kocha wao wa makipa Chlouha Zakaria.

"Lakini Simba italeta kocha mpya wa viungo baada ya kuachana na huyu wa sasa, lengo ni kukiimarisha kikosi kwa sababu uongozi umepania kufanya vizuri msimu ujao," alisema.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Gain', alinukuliwa akisema wanafahamu makosa waliyoyafanya msimu ulioisha hivyo wamejipanga kufanya maboresho makubwa kuanzia kwenye benchi la ufundi.



Wahitimu wa masomo ya Usalama katika ndege wakicheza muziki wakati wa mahafali ya sita ya Chuo cha Usalama wa Ndege cha Precision jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam FC si kwa Yanga

INATOKA UKURASA 24

dhahiri.

Krosi ndefu ya Joyce Lomalisa ilimpita kichwani Musonda ambaye alikuwa amejiandaa kukwamisha wavuni, lakini ukawa mrefu kidogo kwake na ikawa ni salama kwa Azam.

Mafuriko ya mashambulizi langoni mwa Azam yaliendelea, dakika ya tano nusura Bernard Morrison aukwamishe mpira wavuni akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, lakini mpira aliopiga kwa staili ya 'mwezi mwandamo' ulitoka kidogo juu ya lango.

Kipa wa Azam, Iddris Abdulai alifanya kazi ya ziada dakika ya tisa, aliporuka upande wake wa kulia na kudaka shuti la Musonda lililopigwa hatua chache tu kutoka alipo.

Musonda aliyekuwa mwiba mchungu kwa mabeki wa Azam, akicheza nafasi ya ushambuliaji wa kati iliyokuwa inachezwa na Mayele, alikosa bao lingine dakika ya 24, akiwa ndani ya eneo la hatari lakini mabeki wa Azam waliwahi kumzuia.

Kipindi cha pili Azam walionekana kuamka kutoka katika usingizi mzito na nusura wapate bao dakika ya 50 baada ya shuti la Ayoub Lyanga kupanguliwa kwa ustadi na kipa Djigui Diarra.

Azam licha ya kupambana kutaka kurudisha bao hilo, mabeki na viungo wa Yanga walikuwa imara kuondoa hatari zote langoni mwao.

# Michezo

Jumanne Juni 13, 2023

Nipashe



## Sancho anafukuziwa na Spurs

UKURASA 22




Wachezaji wa Yanga wakishangilia ubingwa wa Kombe la Shirikisho (FA) baada ya kuifunga Azam bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali uliochezwa jana Uwanja wa Mkwakani, Tanga. **PICHA: BINZUBERY**

# Azam si kwa Yanga

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Wanalambalamba wameshindwa kuifunga timu hiyo ya Jangwani katika mechi zote tatu za msimu huu. Yabeba FA bila Mayele...

AZAM FC si kwa Yanga! Ndicho unachoweza kusema baada ya timu hiyo ya Chamazi msimu huu kuonekana si lolote kwa Yanga.

Baada ya kushindwa kuifunga Yanga katika mechi mbili za Ligi Kuu msimu huu, jana Azam FC ilikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa mabingwa hao mara 29 wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika mchezo wa fainali ya Kombe la FA ulioshuhudiwa watoto wa Jangwani wakimaliza msimu huu kwa mafanikio makubwa. Wamechukua makombe mawili na kufika fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

**Azam ambayo msimu huu ilionekana kuwa 'moto' katika michuano hiyo ikiiondoa Simba hatua ya nusu fainali kwa kuifunga bao 2-1 na kukata tiketi ya kucheza fainali. Yanga waliowaondoa Singida United katika hatua kama hiyo.**

Msimu huu Azam imeonekana kukwama kwa Yanga ambapo katika michezo mitatu waliyokutana, miwili ya ligi kuu iliambulia pointi moja kati ya sita. Mzunguko wa kwanza walitoka sare ya mabao 2-2, mzunguko wa pili Yanga alishinda kwa mabao 3-2 na mchezo wa jana wa fainali Yanga waliendeleza ubabe kwa ushindi huo wa bao 1-0 lililofungwa na Kennedy Musonda.

Hii inakuwa mara ya pili Azam FC kufungwa na Yanga katika fainali ya michuano hiyo ambapo kwenye msimu wa 2015/16 ilikubali kipigo cha mabao 3-1 katika mechi ya fainali iliyochezwa Mei 25, 2016.

Mchezo wa jana umehitimisha msimu bora zaidi kwa Yanga waliotwaa ubingwa wa Ligi Kuu, pia walikaribia kuchukua ubingwa wa Afrika wa Kombe la Shirikisho baada ya matokeo ya jumla ya mabao 2-2 dhidi ya USM Algers, lakini wakalikosa kombe hilo kwa kanuni za mashindano hayo (goli la ugenini).

Hii inafanya Yanga kuwa timu iliyofanya vizuri zaidi nchini katika mashindano yote iliyoshiriki msimu huu.

Katika mchezo wa jana, Yanga, ikicheza bila mshambuliaji wake hatari, Fiston Mayele aliyeenda kujiunga na timu yake ya taifa, iliandika bao lake dakika ya 13 kupitia kwa Musonda aliyeunganisha kwa kichwa krosi ya Djuma Shaaban kufuatia mpira wa kona fupi uliopigwa na Tuisila Kisinda.

Yanga ilianza mechi kwa kasi na kuishambulia mfululizo Azam, ambayo wachezaji wake walionekana kama hawakujiandaa, kiasi cha sekunde ya 39 tu kunusurika kufungwa bao lililoonekana

INAENDELEA UKURASA 23

## Simba yawatoa hofu mashabiki kuhusu usajili

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya Simba umewataka mashabiki wa klabu hiyo kupuuzia taarifa zisizo sahihi za usajili unaohusisha klabu hiyo katika kipindi hiki ambacho wanakiboresha kikosi chao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema katika kipindi hiki kutakuwa na maneno mengi ya uongo ya klabu hiyo kuhusishwa na wachezaji ambao hawapo kabisa katika malengo ya timu hiyo.

Alisema Simba wanaendesha mchakato wao wa usajili kwa siri kubwa na wanatoa taarifa pale kila kitu kinapokuwa kimekamilika.

"Wanachama na mashabiki wetu wasifuatishe maneno ya mtaani, Simba ni timu kubwa na kwenye suala la usajili linaendeshwa kwa umakini na kila mchezaji tunayemtaka tutampata na kumtangaza pale kila kitu kitakapokamilika," alisema Ally.

Alisema katika kipindi hiki Simba inahusishwa na wachezaji wengi hata wale ambao hawapo kwenye malengo ya timu yao.

"Ukiangalia kwenye mitandao na vyanzo vingine, tetesi zimekuwa zikija kimkakati, lengo ni kuwavuruga wanachama na mashabiki wa Simba, ukiangalia kuna wachezaji ambao hawana

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >